# Kufanywa Wana Wenye Mamlaka #2

Jeffersonville, Indiana, USA

Mei 18, 1960

1 Mimi … nimechelewa kidogo. Nilikuwa na mtu aliyekuwa na vurugu, mkali sana, nami ilinipasa tu kwenda wakati huo, kwa sababu walikuwa, na hali mbaya sana. Nami nikaendesha kote kutokea Michigan, mkuu wa polisi alikuwa ameita, na kadhalika, kwamba walikuwa katika hali mbaya sana. Sasa, lakini itakuwa sawa; kila kitu—kila kitu kiko chini ya mamlaka, kwa hiyo hilo ni sawa. Bwana anapoingia, kila kitu kinakuwa chini ya utawala wakati huo, sivyo? Loo, Yeye—Yeye ni mwema sana; kuwazia wema Wake na rehema Zake, juu ya kile anachomaanisha kwetu, na jinsi sifa Zake zilivyo za thamani.

Vema, tulijaribu kuanza, tukisema ya kwamba tungechukua zile sura tatu za kwanza za Kitabu cha Waefeso. Nami nafikiri tunayo yale maneno matatu ya kwanza, ama matatu ya kwanza ya *kitu fulani* pale. Hatukufika mbali sana, lakini huenda usiku wa leo tunaweza kuendelea mbele kidogo. Sasa, nataka kusema ya kwamba mimi si mwanafunzi wa Biblia, kabisa, na simwanatheolojia, bali ni—ninampenda Bwana, nami napenda kumtumikia na … [Ndugu fulani anazungumza na Ndugu Branham — Mh.]

Mtu fulani, dharura tu, kasema, kabla tu hatujaendelea sasa, msichana mdogo akiwa hospitalini huko Louisville, na mabingwa wote walio bora wamemkatia tamaa, anakufa sasa, na anaomba maombi kwa ajili ya mtoto huyu. Kama Wakristo, ni wajibu wetu kuinamisha vichwa vyetu, sasa, kwa ajili ya maombi.

Bwana wetu mwenye neema, si wajibu wetu pakee bali ni majaliwa yetu, na ni sha—shauku yetu kwamba tunainamisha vichwa vyetu usiku wa leo kama kanisa, kama kundi la walioitwa watoke, watu wanaoamini hapa usiku wa leo, kufundisha Neno Lako, likituweka mahali petu katika ule Mwili, pale ambapo sisi tunapaswa kuwa, na pale ambapo tunaweza kufanya kazi vizuri pamoja kama viungo vya Mwili wa Kristo.

Na sasa tunaitwa sasa tumwendee Mungu mara moja. Na kila mmoja wetu sisi akina baba tunafikiri ya kwamba, vipi kama huyo angekuwa ni msichana wetu mdogo, jinsi mioyo yetu ingechomwa na kuumia ndani yetu, nasi tungeyaita makanisa yafanye maombi mara moja. Na moyo wa baba fulani unachomwa, unauma. Bwana, jalia huo Utu mkuu wa Roho Mtakatifu uje sasa hivi kwenye moyo wa baba huyo. Ondoa kila kivuli cha saka, na kila maumivu, na jalia yeye ajue ya kwamba Wewe ni Mungu na hakuna ugonjwa unaoweza kusimama katika Uwepo Wako wakati agizo Lako la Kiungu limekwishatekelezwa na kanisa Lako na watu Wako.

2 Na kama vile katika juma hili lote, sisi tukiomba, tangu Jumapili iliyopita nimewazia juu ya njia hizi au hali hizi za maombi. Kwa ulimwengu haionekani tuna silaha halisi hasa, lakini kakombeo haka kadogo ni hatari sana kanaposhikiliwa katika vidole vya imani. Ee Bwana, jalia maombi yetu yajibiwe, hayo mauti yannayoning'inia kule juu ya mtoto huyo, na yaangamizwe; lile giza, utusitusi, viondoe kwenye kitanda cha hicho kitoto, huyo mtoto mchanga, au mtoto, msichana mdogo. Na jalia ile Nuru kuu ya Uwepo wa Mungu iangaze juu yake. Jalia atoke kwenye hospitali hiyo, mtoto mwenye afya.

Mungu, tunajua tu huko ng'ambo ya mto wapendwa wetu wanangojea, na ni la utukufu. Lakini sisi tunawapenda watoto wetu wadogo. Nasi tunaomba, Bwana, ya kwamba kwa ajili ya utukufu Wako, ya kwamba utaurehemu uhai wa mtoto huyo. Sisi, kama kanisa Lako, tunayakemea hayo mauti, na kusema, "Simameni kimya kule. Huwezi kumchukua mtoto huyo, kwa sababu tunayadai maisha yake kwa ajili ya ufalme wa Mungu." Tujalie mambo haya, Bwana, yaende moja kwa moja tunakoyaelekeza, katika Jina la Yesu Kristo, Mwokozi wetu. Amina.

3 Tunaamini? Sijui ningefanya nini kama sikuwa Mkristo. Nisingetaka kuishi zaidi. Hakuna kitu cha kuishia, ila kuwafanya wengine waokolewe, ndilo jambo bora sana nijualo.

Sasa, usiku wa leo tunataka tu kuanzisha msingi mdogo wa somo letu lililopita. Nami nitajaribu kusoma, kwa sababu, ile sura nzima, kama nataweza usiku wa leo. Kwa hiyo Jumapili asubuhi itanibidi labda kuingiza ndani Jumapili asubuhi na usiku, kama hilo ni sawa, kujaribu kupata katika taratibu hii ya yale ninayotaka kanisa lione. Loo, ni jambo tukufu sana kuona mahali pako! Na hakuna mtu anayeweza kufanya jambo lo lote isipokuwa ujue vizuri unalofanya.

4 Vipi kama ulikuwa unakwenda kuwa … kufanyiwa upasuaji, na kulikuwako na daktari kijana ambaye ndiyo kwanza atoke shuleni ambaye ange … hakuwahi kufanyiwa upasuaji hapo awali. Hata hivyo, yeye alikuwa kijana na mwenye sura nzuri, na nywele zake zimechanwa zikalazwa maridadi kisasa, naye alikuwa amevalia vizuri sana, kavalia kimaridadi sana, na kila kitu. Naye akasema, "Nimenoa visu, na nimechemsha vyombo vyote na kadhalika." Lakini ungekuwa na wasiwasi kidogo juu ya jambo hilo. Afadhali nipate daktari mzee ambaye alikuwa amefanya upasuaji huo mara nyingi huko nyuma, kabla sijakubali kukatwa. Ni—nataka kumjua mtu fulani si yule aliyetoka shuleni hivi karibuni, nataka mtu aliye na ujuzi fulani.

Na Yule aliye na ujuzi kuliko wote ninayemjua, kumwita usiku wa leo, ni Roho Mtakatifu. Yeye ni Tabibu mkuu na Mwalimu mkuu wa Mungu.

5 Na kwa kuwekea Ujumbe wangu msingi usiku wa leo, bado kutoka kwenye mahubiri ya Jumapili, kwamba ni … Wao walimkataa Samweli aliyekuwa na Neno la Bwana; na kumkubali Sauli, mwana wa Kishi; na kumkataa Samweli, ambaye alimwakilisha Roho Mtakatifu, kwa sababu alinena tu kama Roho alivyomwongoza kunena. Na wakati yeye alipowaelekeza waone jambo hilo, yeye alisema, "Kumbukeni, sijawaambia neno kwa Jina la Bwana ila lile Bwana alilolitimiza. Wala sijaenenda vibaya mbele zenu. Na hakuna mtu awezaye kunishtaki kwa dhambi."

Kama vile Yesu alivyosema, "Ni nani awezaye kunihukumu kwamba nina dhambi?" Unaona?

Naye akasema tena, ya kwamba, "Sijaja kwenu na kuwaombeni fedha na kadhalika. Sijajitwalia chochote kutoka kwenu. Lakini yote niliyosema yamekuwa kwa manufaa yenu, hayo niliyowaletea kutoka kinywani mwa Bwana."

Na watu wote wanashuhudia, "Hiyo ni kweli. Yote hayo ni kweli, bali hata hivyo tunataka kuwa na mfalme. Tunataka kuwa kama walimwengu wengine."

6 Sasa, usiku wa leo, Maandiko yetu yanagawanya Kitabu cha Waefeso, ndicho Kitabu cha Yoshua cha Agano Jipya. Kinawagawia na kuwaweka katika utaratibu "wale walioshinda." Sasa, ni msingi tu kwa dakika chache, kupata mahali kabla hatujaanza kusoma, tukianzia na ile aya ya 3. Sasa, tunaona Jumapili iliyopita usiku ya kwamba … Mungu katika Agano la Kale alikuwa amewaahidi Israeli nchi ya pumziko, kwa sababu walikuwa wamekuwa wasafiri na wenye kutangatanga. Nao walikuwa katika nchi ambayo si yao, na Mungu alikuwa ameahidi kupitia kwa Ibrahimu ya kwamba angeishi ugenini, uzao wake ungekaa ugenini kwa muda wa miaka mia nne kati ya watu wa wageni, na kutendwa mabaya, lakini kwa mkono wenye nguvu Yeye angewatoa huko akawaingize katika nchi nzuri iliyojaa maziwa na asali.

7 Na, sasa, wakati wa ile ahadi ulipokaribia, Mungu alimwinua mtu fulani awapeleke kwenye nchi hiyo. Ni wangapi darasani usiku wa leo huyo alikuwa nani … wanaojua huyo alikuwa ni nani? Musa. Angalia, mfano halisi kabisa wa Yule wetu aliyetolewa kutuleta kwenye Nchi ya ahadi, Kristo. Sasa tunayo ahadi, maana ahadi yetu ni Pumziko la kiroho, ambapo, lao lilikuwa ni pumziko la kimwili. Na kwa hiyo wao walikuwa wakija kwenye nchi ambayo wangeweza kusema, "Hii ndiyo nchi yetu, sisi si wenye kutangatanga tena tumetulia, hii ni nchi yetu, na hapa tuna pumziko. Tutapanda mahindi yetu, mashamba yetu ya mizabibu, na tutakula kutoka kwenye mashamba yetu ya mizabibu. Na kisha tutakapoaga dunia, tutawaachia watoto wetu."

8 Loo, jinsi tungeweza kuingia katika ardhi yake, sheria za urithi, kama vile Naomi na Ruthu, Boazi. Tuyarudishe hayo yote. Jinsi ambavyo ndugu katika Israeli, jinsi ambavyo hana budi … cho chote alichokuwa amepoteza hakina budi kukombolewa na jamaa aliye wa karibu. Loo, ni zuri iliyoje! Ingechukua majuma na majuma na majuma na majuma, tusingeondoka kwenye hii sura, tukiingilia jambo hilo. Tungeweza kuunganisha Biblia nzima papa hapa, papa hapa katika sura hii moja.

Na, loo, napenda tu kulisoma Hilo. Tulizoea kuichukua, na kuichukua kwa mwaka mmoja na nusu, na kamwe tusiondoke kwenye hicho Kitabu. Tunakaa tu moja kwa moja Nacho.

9 Sasa, lakini, lilikuwa ni jambo kuu sana hivi kwamba urithi, jinsi ilivyokuwa kwamba urithi katika nchi ambao hapana mtu isipokuwa jamaa aliye wa karibu angeweza kuukomboa huo urithi. Sasa, hebu niingize tu jambo dogo muhimu hapa nililoligusia hivi majuzi usiku, kwenu akina mama. Ni wangapi hapa wamewaombea wapenzi wao, waliopotea? Vema. Haya basi tena, mnaona, "Urithi wenu." Mnaona?

Paulo alimwambia yule Mrumi, akasema, "Mwamini Bwana Yesu Kristo, nawe pamoja na nyumba yako mtaokolewa." Kama una imani ya kutosha kwa ajili ya kuokolewa wewe binafsi, uwe na imani ya kutosha, haidhuru mvulana huyo ni mpotovu jinsi gani, ama msichana huyo alivyopotoka, wataokolewa kwa vyovyote. Mungu, kwa namna fulani! Kama ikimlazimu kuwalaza chali, wakilala mle hospitalini, wakifa, wataokolewa. Mungu aliahidi jambo hilo. Ule urithi! Loo! "Nao watakuwa kule," Isaya alisema, "na watoto wao wote pamoja nao. Hawatadhuru wala hawataharibika katika mlima Wangu wote mtakatifu, asema Bwana."

Loo, nina sehemu ndogo ambayo natumaini naweza kuifikia usiku wa leo, kwa ajili yenu. Inachoma tu moyoni mwangu, ya jinsi hilo linavyokuwa hivyo.

10 Lakini sasa, tusonge mbele. Basi je! Ulimwona Musa, yule mtenda miujiza mashuhuri aliyewaleta Israeli kupitia ile nchi, na kuwaleta hata kwenye nchi ya ahadi, lakini yeye hakuwapa urithi wao? Yeye hakuwapa urithi wao; aliwaongoza hadi kwenye ile nchi, lakini Yoshua ndiye aliyewagawia hao watu ile nchi. Sivyo? Naye Kristo alililеta kanisa kufikia mahali ambapo waliandaliwa milki yao, walipewa, ikisalia tu kuvuka Yordani, bali Roho Mtakatifu Ndiye anayeliweka kanisa katika utaratibu. Yoshua wa leo hii analiweka kanisa katika utaratibu wake, akimpa kila mmoja, karama, mahali, cheo. Naye ndiye Sauti ya Mungu ikinena kupitia kwa yule mtu wa ndani ambaye Kristo amemwokoa, Roho Mtakatifu. Sasa mnafahamu umbali huo? Sasa tunaingia katika Kitabu cha Waefeso. Sasa, vivyo hivyo, Yeye anaweka kanisa mahali pao. Sasa, Yoshua aliwaweka katika nchi ya kawaida. Sasa Roho Mtakatifu analiweka

kanisa, mahali pake, katika nchi, ili kwamba wao, katika mahali ambapo ni pao, urithi wao.

11 Sasa, jambo la kwanza analoanza nalo hapa, anaandika barua yake, "Paulo." Ambalo, tutaona baada ya kitambo kidogo kwamba fumbo hili lote lilifunuliwa kwake, si katika seminari, si kwa njia ya mwanatheolojia ye yote, bali ilikuwa ni ufunuo wa Kiungu wa Roho Mtakatifu ambao Mungu alimpa Paulo. Tukijua kwamba fumbo la Mungu, yeye alisema, ambalo liliyokuwa limefichwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, lilikuwa limefunuliwa kwake na Roho Mtakatifu. Na Roho Mtakatifu miongoni mwa watu alikuwa akimweka kila mmoja katika utaratibu, akiliweka kanisa mahali pake.

12 Sasa, jambo la kwanza ambalo Paulo anaanza hapa kuwaambia watu, ni kuchukua ninii yote … Kumbukeni, hili ni kwa kanisa, si kwa mtu aliyeko nje. Kwake ni fumbo katika mafumbo kwake, hawezi kulielewa kamwe,linamshinda akili, hajui kitu hata kidogo juu yake. Lakini, kwa kanisa, ni asali ndani ya mwamba, ni furaha isiyotamkika, ni dhamana iliyobarikiwa, ni nanga ya nafsi, ni tumaini na tegemeo letu, ni Mwamba wa Nyakati, loo, ni kila kitu kilicho chema. Kwa maana mbingu na nchi zitapita, bali Neno la Mungu halitapita kamwe.

13 Lakini mtu aliye nje ya Kanaani hajui kitu juu yake, angali anatangatanga. Si kusema ya kwamba yeye si mtu mzuri, sisemi hivyo. Sisemi mtu aliye Misri si mtu mzuri, bali yeye, hadi awe ameingia kwenye milki hii.

Na hiyo milki, ambayo, ile ahadi iliyotolewa kwa kanisa si nchi ya kawaida, bali ni nchi ya kiroho, kwa kuwa sisi ni ukuhani wa kifalme, taifa takatifu. Ndipo katika ukuhani huu wa kifalme, taifa takatifu, watu wa kipekee, walioitwa watoke, waliochaguliwa, wakatengwa, waliotengwa, ndipo ulimwengu wote umekufa upande wa nje. Nasi tunaongozwa na Roho. Wana na binti za Mungu wanaongozwa na Roho wa Mungu; si na mwanadamu, bali kwa Roho.

14 Yote katika upendo, kitu hicho chote kimeunganishwa pamoja sasa. Hili jambo limejaribiwa kufundishwa mara nyingi, na hapana shaka wanatheolojia mashuhuri wameliingilia kindani zaidi kuliko ambavyo ningaliweza mimi. Lakini jambo ninalotaka kujaribu kuwaletea ni hili, ya kwamba mtu aliye katika Kristo, mwneye Roho Mtakatifu, anaweza kuchukuliana na mtu huku amekosea, mvumilivu, mwenye upole, mwenye subira. Yeye ni mzuri, mnyenyekevu, mwaminifu, amejazwa na Roho, hawi hasi kamwe, yuko chanya daima. Yeye ni mtu tofauti.

Si mtu tu ambaye, "Wakati mmoja tulikuwa nayo. Kama tulipaza sauti, tuliipata, sisi Wamethodisti. Loo, tulipopaza sauti, tulikuwa katika ile Nchi." Hilo ni zuri, hilo ni sawa, naamini hivyo pia.

Ndipo Wapentekoste wakaja wakinena kwa lugha, wao, "Waliipata; kila mtu aliyenena kwa lugha aliipata." Ninaamini hivyo, pia. Lakini hata hivyo tuliona ya kwamba wengi wao hawakuipata Hiyo bado, unaona. Unaona? Sasa wao ni …

15 Sasa tunafikia kwenye hili fumbo kuu liliyofichwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu na sasa linafunuliwa katika siku za mwisho kwa wana wa Mungu. Mnaamini jambo hilo kuwa ni kweli, ya kwamba wana wa Mungu wanadhihirishwa? Kabla hata hatujaenda popote, hebu na tufungue Warumi sura ya 8 kwa muda kidogo tu, hebu niwasomeeni jambo fulani. Tuone kama hili halifikii yale ninayoyanena hapa. Sasa tutafungua Warumi 8, aya ya 19 ya—ya sura ya 8 ya Warumi.

> *Kwa maana viumbe vyote … vinatazamia kwa shauku nyingi* madhihirisho *ya wana wa Mungu.*

16 Kwa matarajio ya dhati, viumbe vyote vinatazamia huo udhihirisho. Unaona, huo udhihirisho! Udhihirisho ni nini? Kufanya wajulikane!

Ulimwengu mzima. Waislamu kule, wanakutazamia. Pande zote, kila mahali, wanakutazamia. "Wako hawa wako wapi?" Tumekuwa na ninii … Tumekuwa na upepo wenye nguvu unaovuma ukienda kasi, tumekuwa na ngurumo na umeme, tumekuwa na mafuta na damu, tumekuwa na mambo ya kila namna; lakini tulishindwa kuisikia ile Sauti ndogo ya utulivu iliyomvutia yule nabii, ambaye alijifunika joho na kutoka, kasema, "Mimi hapa, Bwana." Unaona?

17 Sasa viumbe vyote vinaugua na kungojea kule kudhihirishwa kwa wana wa Mungu. Sasa, Paulo kwanza ataliweka kanisa mahali pake hasa. Sasa ili tu kupata msingi, hebu na tusome tena.

> *Paulo, mtume wa Yesu Kristo kwa mapenzi ya Mungu, kwa watakatifu* (hao ni wale "walio watakatifu") *walioko Efeso, na … walio wanaomwamini Kristo Yesu;*

Sasa, kusudi darasa lisisahau jambo hilo, tunaingiaje katika Kristo? Je! Tunajiunga na kanisa kuingia katika Kristo? Je! Tunakiri kusudi tuingie katika Kristo? Je! Tunatumbukizwa majini kusudi tuingie katika Kristo? Tunaingiaje katika Kristo? Wakorintho wa Kwanza, sura ya 12, "Kwa maana kwa Roho mmoja," mmoja, herufi kuu R-o-h-o, ambaye ni Roho Mtakatifu, "sisi sote tumebatizwa kuwakatika Nchi ya ahadi."

18 Katika Nchi hii ya ahadi, kila kitu ni mali yetu katika Nchi ya ahadi. Unaona jambo hilo, Ndugu Collins?

Unaona, kila kitu katika Nchi ya ahadi! Wakati Israeli walipovuka huu Yordani, kuingia katika nchi ya ahadi, walishinda kila kitu!

Sasa kumbukeni, katika Nchi hii ya ahadi, hiyo haimaanishi kwamba unayo kinga ya magonjwa, hiyo haimaanishi ya kwamba una kinga ya shida. Lakini linamaanisha jambo hili, (loo, hebu hili lizame ndani), linasema hivi, ya kwamba ni yako! Inuka tu ukaitwae! Unaona? Wakati …

19 Na, kumbukeni, njia pekee ambayo Israeli walipata kumpoteza mtu, ni wakati dhambi ilipoingia kambini. Hiyo ndiyo njia pekee tunayoweza kupoteza u—ushindi, ni kwa dhambi kuingia kambini, kasoro fulani mahali fulani. Wakati Akani alipoiba ile kabari na joho lile la Kibabeli, dhambi ilikuwa kambini, na vita vikaenda vibaya.

Hebu nipe kanisa hili—hili usiku wa leo, kundi hili la watu, kikamilifu, lililo ndani ya ahadi za Mungu kikamilifu, wakiwa na Roho Mtakatifu, wakitembea katika Roho, nasai ugonjwa wowote au mateso yoyote, ama cho chote kilichopo, kila Joe Lewis kaliye nchini, pamoja na ukafiri wake wote, na wasioamini wote waliopo, kuingiza ugonjwa wowote au mateso katika mlango huu, nao watatoka hapa wakiwa wazima kabisa. Naam, bwana. Mungu alitoa hiyo ahadi, ni dhambi tu ya kutokuamini inayoweza kuizuia. Sasa tutaona hii dhambi ndogo ni nini, baada ya kitambo kidogo, sasa.

… Walio *katika Kristo Yesu:*

*Neema na iwe kwenu na amani zitokazo kwa Mungu Baba yetu na ... Bwana Yesu Kristo.*

*Atukuzwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, aliyetubariki kwa baraka zote za rohoni, katika sehemu za kimbinguni ndani yake Kristo, ndani—ndani yake katika Kristo.*

20 Tunapokuwa katika Kristo, tuna baraka ya kiroho. Nje ya Kristo, tuna mihemuko. Katika Kristo tuna baraka halisi. Si kuamini kwa kujifanya, si kujisingizia, si kuigiza. Lakini mradi tu unajaribu kusema kwamba uko katika Nchi ya ahadi, nawe hauko, dhambi zako zitakufichua. Na, muda si muda unajua, utajikuta mwenyewe unatatanika na—na kadhalika, kama tunavyokuita ulimwenguni, umevurugikiwa. Utaona ya kwamba huna kile unachozungumzia. Lakini unapokuwa katika Kristo Yesu, Yeye amekuahidi amani ya Kimbinguni, baraka za Kimbinguni, Roho wa Kimbinguni, kila kitu ni chako. Wewe uko katika Nchi ya ahadi na umemiliki kabisa kila kitu. Amina. Linapendeza iliyoje! Loo, hebu na tujisome.

*Kama vile alivyotuchagua …*

Sasa, hapa ndipo kanisa linapojikwaa vibaya sana.

*Kama vile alivyotuchagua katika yeye …* (Katika Nani?) Kristo.

21 Tunaona sasa, huko nyuma katika—katika Mwanzo na katika Ufunuo, Ufunuo 17:8, ya kwamba Yeye alituchagua katika Kristo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Sasa, neno … Hebu nisome inayofuata.

*… misingi ya ulimwengu, ili tuwe watakatifu, watu wasio na hatia mbele zake …*

*Kwa kuwa alitangulia kutuchagua …*

Sasa nataka kusimama penye hilo neno "alitangulia kutuchagua." Sasa, *alitangulia kutuchagua* si kusema, "Nitamchagua Ndugu Neville, na si—si—si—si-sitamchagua Ndugu Beeler." Si hivyo. Ni kule kujua tangu zamani kwa Mungu ambako alijua ni yupi angekuwa sahihi na ni yupi hakuwa sahihi. Kwa hiyo, kwa kujua tangu zamani, Mungu akijua kile atakachofanya, Yeye alitangulia kuchagua kwa kujua Kwake tangu zamani kusudi afanye mambo yote yatende kazi pamoja kwa manufaa ya hao wampendao Mungu, kusudi Yeye apate, katika wakati ujao, kuvikusanya vitu vyote pamoja. katika Mmoja, ambaye ni Kristo Yesu.

22 Hebu niwachoreeni mfano mdogo hapa. Ni mzuri. Tunarudi nyuma, naamini nilizungumzia jambo hilo kidogo hivi majuzi usiku, ama kuligusia, katika Mwanzo, sura ya 1, 1:26, wakati Mungu alipojiita Jina Lake, "Bwana Mungu," liko katika neno la El, Elah, Elohim, ambalo linamaanisha "Yeye aishiye peke Yake." Hapakuwepo na kitu kingine kilichokuwepo ila Yeye. Hakukuwa na hewa, hakukuwa na nuru, hakukuwa na nyota, hakukuwako na ulimwengu, hakukuwa na kitu kingine chochote. Ilikuwa ni Mungu, na Mungu peke Yake, El, Elah, Elohim. Sasa, Yeye alifanya hilo.

23 Ndani yake kulikuwa na sifa ambazo zilimaanisha ya kwamba Yeye alikuwa … Ndani ya huyu El mkuu, Elah, Elohim kulikuwa na sifa ama … Mnajua *sifa* ni nini, ama hebu niliseme namna hii, kulikuwa na "asili." Hiyo ni kusudi huyo jamaa huyo mdogo alielewe, nami ni mmoja wa jamaa wadogo wanaopaswa kulifahamu kwa jia hiyo. Ndani Yake kulikuwemo na asili ya kufanyika baba, lakini Yeye huishi peke Yake, hakuna kitu cha kumfanya Baba. Na, sasa, mle ndani ya hiyo mlikuwa na kitu kingine, kwamba Yeye alikuwa Mungu; na mungu ni kitu cha kuabudiwa; bali Yeye alikuwa akiishi peke Yake, El, Elah, Elah, Elohim, kwa hiyo hakukuwako na kitu cha kumwabudu. Ndani mle, Yeye alikuwa Mwokozi, wala hakukuwako na kitu kilichopotea kiokolewe. Unaona? Ndani mle, Yeye alikuwa Mponyaji, unaona, bali hakukuwako na kitu cho chote cha kigonjwa kiponywe, wala cho chote cha kuugua. Sasa mnaipata hiyo

picha? Kwa hiyo sifa Zake, asili Yake ilisababisha mambo yalivyo leo.

24 Watu wengine husema, "Vema, kwa nini Mungu hakuisitisha hapo mwanzo?" "Yeye ni mkatili mwenye moyo wa kinyama," kasema Joe Lewis, yule aliyemlaumu Joe, ama Jack Coe, unaona. Kasema, "Yeye ni mkatili tu mwenye moyo wa kinyama. Hakuna kitu kama Mungu. Kama kungekuwako na kitu kama hicho, Yeye angekuwa …" Loo, mimi … alimwita tu kila namna ya majina, unaona. Lakini ni kwa sababu tu huenda akawa na maarifa mengi mno *hapa* juu, bali hana kitu *hapa* chini.

Sasa, hapo, hivyo ndivyo ilivyo. Unaona? Neno hili linasema jambo hili hapa, Naye amelificha. Na mafumbo haya yamefichwa sasa, kumbukeni, Biblia ilisema, "Tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, zikingojea madhihirisho ya wana wa Mungu," kuziweka wazi kwa kanisa. Loo, jamani! Mnalipata?

25 Sasa naiacha hadithi yangu kidogo tu, au nitaleta … Nitaenda kwenye wazo langu linalofuata ili kupata hili. Sasa kumbukeni, kote katika nyakati za Musa, huko nyuma katika nyakati za manabii, huko nyuma katika nyakati zote, wamengojea mpaka siku hizi za baadaye mambo haya yapate kuonyeshwe wazi, kulingana na Maandiko. Hiyo ni kweli, kwa ajili ya kufunuliwa kwa wana wa Mungu. Kwa nini? Kutoka kwa waliopotea … mpaka kama ile piramidi, kama nilivyosema, ikijengwa na kuanza kuwa nyembamba zaidi, na zaidi, na zaidi.

26 Kama vile nilivyotoa tamshi hili mara nyingi, na kusema, Mungu alifanya Biblia tatu. Ile ya kwanza, Yeye aliiweka angani, ile zodiaka. Je! Ulipata kuona zodiaka? Umbo la kwanza katika zodiaka ni nini? Bikira. Umbo la mwisho ni nini katika zodiaka? Leo yule simba. Yeye alikuja mara ya kwanza kwa bikira, Yeye anakuja mara ya pili kama Simba wa kabila la Yuda. Unaona?

Yeye aliifanya ya pili katika piramidi, huko nyuma katika siku za Henoko, wakati walipojenga piramidi. Nao huzipima. Sielewi hilo. Lakini kwenye vita, ambapo wanainama na kwenda kwa magoti yao kwa muda mrefu, na wanaweza kupima umbali wa vita. Mnajua wamefikisha kipimo wapi sasa? Moja kwa moja kupitia kwenye chumba cha mfalme. Na wakati hii piramidi ilipokuwa inajengwa … Hatungeweza kuijenga, kwa kila kitu tulicho nacho leo. Hatungeweza kuijenga.

27 Imejengwa moja kwa moja namna *hii*, kufikia hatua fulani. Na lile jiwe lililo juu … Lile jiwe la kifuniko halikupatikana kamwe. Wao kamwe hawakuweka kifuniko juu ya hiyo piramidi. Sijui kama mnajua hilo ama hujui, ile piramidi kubwa ya Misri, kamwe haikuwa na jiwe la kufunika. Kwa nini? Lile jiwe la kifuniko lilikataliwa, Kristo, lile Jiwe la Kichwani, unaona, alikataliwa.

Lakini tunapokua kutoka kwenye wakati wa Kilutheri, wakati wa Kibatisti, wakati wa Kimethodisti, wakati wa Kipentekoste, tuko moja kwa moja kwenye lile Jiwe la kifuniko sasa, unaona, tukingojea na kutamani hilo Jiwe la kukokota liwekwe,hilo jengo likamilike. Hivi hamjasoma katika Maandiko, "Lile jiwe lilikataliwa"? Bila shaka, tunatambua ya kwamba hilo lilikuwa likizungumzia hekalu la Sulemani. "Lakini lile Jiwe lililokataliwa limekuwa ndilo Jiwe kuu la pembeni." Nami nasema jambo hili ili tu niwape pi—pi—pi—picha yake.

Sasa, na katika Biblia, tunaishi katika siku ya mwisho, kwenye kilele cha piramidi, wale samaki waliokingamana wa wakati wa kansa katika zodiaka, katika wakati wa kuja kwa Leo yule simba, katika kuwekwa kwa jiwe la kifuniko, na katika siku za madhihirisho ya wana wa Mungu, katika Biblia, unaona. Mnaona mahali tulipo? Tuko kwenye wakati wa mwisho kabisa.

28 Ni wangapi wamekuwa wakisoma gazeti juma hili, kile Khrushchev na hao wengine waliyosema? Loo, wako tayari; na sisi pia. Amina. Tayari! Ni sawa, mnaona. Loo, ni—ni—ni majaliwa jinsi gani, ni siku ya jinsi gani! Laiti Wakristo wangalitambua siku tunayoishi. Jamani!

Unaonaje? Mwandishi wa Kitabu hiki, aliyeiona, na kuona mahali ambapo jambo hili litadhihirishwa katika siku za mwisho, akingojea na kuugua kwa ajili ya hao wana wa Mungu kuinuka katika siku za mwisho, kwa nguvu za Roho Mtakatifu mwishoni mwa wakati, kufunua mambo ya siri tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, kuyafichua.

29 Sasa hebu na turudi kwenye "msingi wa ulimwengu" tena, kupata ufunuo, tuone kama tuko sahihi au la. Ninatumaini sijifanyi mwenyewe kukufuru kwa kumwita Mungu, "Baba," bali nataka kulisema namna hiyo ili mpate kulielewa. Baba! Baba alitaka watoto, kwa hiyo alifanya nini? Yeye alisema, "Na kuwe na Malaika." Nao wakamzunguka. Loo, hilo ni sawa. Wao wakamwabudu, ndipo Yeye alikuwa Mungu, zile sifa. Kumbukeni, Yeye alikuwa El (El), Elah, Elohim, anayeishi peke yake, hakuna kitu ila Yeye. Kitu cha kwanza kutokea kilikuwa Malaika. Halafu, Malaika hawangeweza kufanya kitu ila kuabudu. Hao hawangalipotea. Kwa hiyo, wasingeweza kuwa wagonjwa, walikuwa ni viumbe visivyopatikana na mauti. Kwa hiyo, Yeye asingeweza kuonyesha uwezo Wake wa uponyaji, asingeweza kuonyesha wokovu Wake. Kwa hiyo basi, kabla, sasa hebu …

30 Ndipo baada ya hayo, Yeye akasema, "Tutatengeneza kitu fulani kinachogusika." Kwa hiyo akaifanya nchi. Na wakati alipoifanya nchi, Yeye akaumba viumbe vyote vya nchi, na kisha akamfanya mtu. Kila kitu kilichotoka ardhini; akianza na—na kiumbe kidogo kabisa ama samaki aina ya yavuyavu, namna tu ya

nyama inayoelea juu ya maji, ilianza paleo, ikafikia … kutokea hapo hadi chura, ambacho ndicho aina ya kiumbe chenye uhai cha hali ya chini sana tunachoweza kupata, wao wanadai, ni chura. Cha hali ya juu kabisa ni mwanadamu. Kutoka kwenye chura akatokea mjusi, toka mjusi na kuendelea na kuendelea na kuendelea, na kila wakati Roho Mtakatifu alipoanza "whooosh," kupulizia, uhai ukaja tena; "Whooosh," uhai wa hali ya juu zaidi. Na jambo la kwanza, kitu fulani kikajitokeza katika mfano wa Mungu, huyo alikuwa ni mwanadamu. Hakuna kitu kilichowahi kuwako, kilichokuwako kamwe, kitakachoumbwa tena, kitu cho chote kilicho cha hali ya juu kuliko mwanadamu, kwa sababu mtu yuko katika mfano wa Mungu. Unaona? Kisha mwanadamu …

31 Wakati Yeye alipomfanya mtu Wake wa kwanza. Sasa, wakati alipovifanya viumbe Vyake vya Kimalaika … Yeye alimfanya mtu, "Aliwaumba mwanamume na mwanamke," wote wakiwa kitu kimoja. Yeye alikuwa wote wawili mwanamume na mwanamke, wa kike na wa kiume. Wakati alipomfanya Adamu na kumweka katika mwili … kumbukeni katika Mwanzo 1, Yeye alimfanya mwanamume na mwanamke. Na katika Mwanzo 2, hapakuwepo na mtu wa kuilima ardhi bado, mtu wa mwili. Hakuna mtu ambaye angeweza kushika kitu chochote na kuilima ardhi, lakini hata hivyo kulikuwako na mtu katika mfano Wake. "Na Mungu ni …" [Kusanyiko linasema, "Roho" — Mh.]. Hiyo ni kweli. Unaona? Yeye alimfanya mtu wa kwanza, "mwanamume na mwanamke aliwaumba." Sasa, wakati alipomfanya mtu wa kwanza!

32 Sasa, kumbukeni, yote pamoja Yeye alikuwa nayo katika nia Yake. Na Jumapili usiku nilielezea hayo. Ne—neno ni wazo lililodhihirishwa. Mungu aliwazia jinsi ambavyo angeweza kuwa Mungu, jinsi angeweza kuabudiwa, jinsi ambavyo angeweza kuwa Mponyaji, jinsi ambavyo angeweza kuwa Mwokozi; na mara aliponena Neno, ilikwisha milele. Loo, laiti hawa wana wa Mungu sasa wanaweza tu kulishika Neno hilo namna hiyo. Mungu anaponena Neno, imekwisha! Kabisa! Huenda alingojea … Mpangilio wa matukio kutokana na wakati yalipotokea unasema ya kwamba, ama mtaalamu wa mambo ya kale na wengine wote, wao wanadai kwamba labda ulimwengu ulikuwa mamilioni na mamilioni na milioni. Sijui, huenda ilikuwa ni matrilioni na matrilioni ya miaka. Sijui ilikuwa muda gani. Mungu hayupo katika wakati. Kwake haijapungua dakika moja tangu aliponena jambo hilo. Yeye angali Mungu. Hakuna wakati Kwake.

Kamwe sikujua jambo hilo namna hiyo mpaka hivi majuzi usiku, majuzi asubuhi, ndiyo namaanisha. Milele, hakuna jana, hakuna kesho, yote ni sasa. Je! Ulipata kutambua neno "MIMI NIKO"? Si "Nilikuwa" ama "Nitakuwa." Ni la Milele, "MIMI NIKO!" Unaona, "MIMI NIKO," daima!

33 Sasa, lakini Yeye alitaka kuweka mambo katika wakati. Ilimbidi kufanya kitu fulani kusudi kiabudu, kwa hiyo sifa Zake zikafanya kitu hiki. Ndipo akamfanya mtu. Ndipo, katika mtu huyu, alionekana mpweke. Kwa hiyo, sasa, kuonyesha sasa nia Yake kuu, kile Yeye alichokuwa nacho katika picha ya Kristo na Kanisa, Yeye hakuchukua kipande tofauti cha udongo na kumfanya mwanamke, bali alitoa kutoka ubavuni mwa Adamu, ubavu; na kutoa kutoka kwenye roho ya Adamu, ile ya kike, na kuiweka katika ubavu huu. Unapomwona mwanamume anayetenda kama jike, kuna kasoro fulani. Na unapomwona mwanamke anayetaka kutenda kama mwanamume, kuna kasoro fulani. Unaona, kuna kasoro fulani. Wao ni roho mbili tofauti, kwa jumla. Lakini, wote pamoja, wao wanafanya kitu kimoja, "hawa wawili ni mmoja." Kwa hiyo Yeye aliwaumba mwanamke na mwanamume, nao hawakupaswa kamwe wazeeke, wase, wapate mvi, la hasha. Walikula, walikunywa, walilala, kama tu tunavyofanya sisi, bali hawakujua kamwe dhambi ilikuwa nini.

34 Sasa nitapita papa hapa kwa ajili ya somo lingine wakati mwingine, juu ya uzao wa nyoka. Ambalo, waliniomba nizirudishe hizo. Lakini hebu nimwone mtu fulani akija na kunionyesha kitu vinginevyo. Hilo ndilo ninalotaka kujua, mnaona.

Sasa, lakini basi baada ya haya yote, ndipo dhambi ilipoingia, ni kitu gani kinachotukia?

Kule juu kabisa, juu, maili milioni moja, milioni mia moja, kuna nafasi kubwa *hivi*, na huo ni upendo mkamilifu wa agape. Kila wakati unapopiga hatua upande *huu*, hupungua inchi moja. Nanyi mnajua jinsi ungekuwa mdogo vipi wakati utakapofika duniani. Ni kivuli cha kivuli cha vivuli. Huo ndio ulio nao, huo ndio nilio nao, kivuli cha kivuli cha vivuli vya upendo wa agape.

35 Kuna kitu fulani ndani yako, kuna kitu ndani ya kila mwanamke hapa aliyezidi umri wa miaka ishirini, kuna kitu ndani ya kila mwanamume hapa aliyezidi umri wa miaka ishirini, ambacho kingetamani kudumu. Una miaka mitano tu, hiyo ni kutoka miaka kumi na mitano hadi ishirini. Baada ya ishirini unaanza kufa. Lakini, kutoka miaka kumi na mitano, wewe ni mtoto tu katika ujana mpaka wakati huo. Na halafu unapevuka kufikia umri wa miaka ishirini. Na baada ya ishirini, loo, unasema, "Mimi ni mtu mzuri tu vile vile." Unasema tu hivyo, bali sivyo ulivyo. Unakufa na unaungua, haidhuru unafanya nini. Mungu alikufanya hata kwenye umri huo, lakini hata hivyo utakufa. Sasa inakuwaje? Sasa unaanza kufa, lakini mle ndani kuna kitu ndani yako kinachosema, "Ninataka kuwa na umri wa miaka kumi na minane tena."

36 Sasa nataka kuwaulizeni jambo fulani. Vipi kama ulizaliwa miaka mia tano iliyopita, nawe ukabakia na umri wa miaka kumi na minane mpaka leo? Ungekuwa kitu cha zamani za kale, pamoja na mawazo yako ya miaka mia tano iliyopita! Kabla wale wazee waanzilishi hawajaja hapa, nawe ulikuwa mwanamke kijana mwenye wazo la namna hiyo. Mbona, ni bora ungeendelea tu ukawa mzee na kuishi miaka mia tano.

Unaona, kuna kasoro fulani.

Unasema, "Vema, sasa hivi ninajisikia vizuri sana, Ndugu Branham. Loo, mimi—mimi—mimi nina umri wa miaka kumi na minane, nina umri wa miaka kumi na sita, ninajisikia vizuri." Mpenzi, hebu nikwambie jambo fulani. Unajuaje ya kwamba mama yako yu hai dakika hii, kama hayuko humu kanisani? Unajuaje kama rafiki mpenzi wako wa kiume hakuuawa tu dakika chache tu zilizopita, ama rafiki mpenzi wako wa kike? Unajuaje kama asubuhi hutakuwa maiti nyumbani mwako? Unajuaje utaondoka kanisani usiku wa leo, ukiwa hai? Ni mambo yasiyo na uhakika sana. Hakuna chenye uhakika. Kama una umri wa miaka kumi na mitano, kumi na miwili, kumi na tisa, sabini na mitano, ama tisini, kuna … kila kitu hakina uhakika. Hujui unakosimama. Lakini hata hivyo unatamani kurudi nyuma kwenye umri wa miaka kumi na tano, kumi na nane. Ni kitu gani kinachokufanya ufanye hivyo?

37 Sasa, kama ukirudi kwenye umri wa miaka kumi na minane na ubakie hapo, na kamwe usiwe mgonjwa wala usiwe … ingekubidi kuwa pamoja na watu wengine, kwa sababu ungeliishi zaidi yao, unaona. Watu wangeendelea katika nyakati zingine nawe ungekuwa ni kitu cha kale. Ingekuwa vibaya zaidi kwako kuliko vile ingekuwa kama ungelizeeka pamoja nao. Lakini kuna kitu kinachokuita uwe kule. Hicho ni yule agape mdogo, kile kivuli kidogo kinachokufanya … Kitu fulani hapa juu.

38 Sasa, hivi majuzi usiku, ama asubuhi ya hivi majuzi, kwenye saa moja, wakati Roho Mtakatifu, kwa wema Wake na neema Yake, alinitwaa kutoka kwenye mwili huu, naamini, naamini. Ndiyo au la, sisemi mimi, na nikaingia katika nchi hiyo na kuwaona watu hao, nao wote walikuwa vijana. Nami nikawaona watu wenye sura nzuri sana niliopata kuwaona maishani mwangu. Naye akaniambia, "Baadhi yao walikuwa na umri wa miaka tisini. Hao ni waongofu wako. Si ajabu wanapaza sauti, 'Ndugu yangu! Ndugu yangu!'"

Sasa, huo ni mwili wa kimbinguni, kwamba tunapokufa hatufanyiki hadithi ya kubuniwa, tunafanyika mwili. Kama sisi tungekuwa, kila mmoja, akifa, kama kombora la atomiki lingetulipua kwenye hii dakikai, mnamo dakika tano kutokea sasa tungekuwa tunapeana mikono sisi kwa sisi na kukumbatiana, na kupaza sauti na kupiga makelele na kadhalika, na kumtukuza Mungu! Naam, bwana. Na Ndugu na Dada Spencer wanaoketi hapa, nadhani ndio wanandoa wenye umri mkubwa zaidi ya wote humu, watakuwa na umri wa miaka kumi na minane, miaka ishirini. Ndugu Neville angekuwa tu mvulana mdogo, nami ningekuwa mtoto mdogo. Nasi sote tungekuwa tu … Hiyo ndiyo hii Kweli kabisa. "Kama maskani hii ya kuishi iliyo ya dunia hii ikiharibiwa, tunayo nyingine ambayo tayari inayongojea."

39 Wakati mtoto mchanga anaposhuka kutoka kwa mama yake, kama kuzaliwa kwa kawaida, mwili wake mdogo unajisokota tu na miguu ikirukaruka, na kadhalika. Samahani kwa tamshi hilo, enyi vijana wanawake. Lakini, anapofanya hivyo, misuli yake iliyo hai inachezacheza. Lakini anapokuja duniani, jambo la kwanza, lanapumua, na kuna mwili wa kiroho wa maumbile unaoingia ndani ya mtoto huyo mchanga papo hapo. Achana naye, atakiinua kichwa chake kidogo na kujisukumiza kwenye matiti ya mama yake na kuanza kunyonya. Kama hakufanya hivyo, hata hayo maziwa hayangelishuka.

Je! Ulipata kuona ndama wakati anapozaliwa, yeye … mara anapoweza kupata nguvu za kutosha kusimama kwa miguu yake? Ni nani anayemwambia? Anazunguka moja kwa moja kwa mama yake, anaanza kujisukumiza na kuanza kunyonya. Loo, naam!

40 Kwa kuwa, wakati mwili huu ulio wa dunia hii unapoletwa hapa, kuna mwili wa kiroho ulio tayari kwa ajili yake. Na mara huu … Loo, haleluya! "Na kama maskani hii iliyo ya dunia hii tunamokaa ikiharibiwa, kuna mmoja unaongojea kule ng'ambo." Mara tu tunapotoka kwenye huu, tunaingia katika huo; ule ambao haitaki kunywa maji baridi, hauhitaji kunywa maji; ule ambao hauli, hiyo si ya mavumbi ya dunia. Lakini hiyo ni halisi tu, na inaweza kuhisi na kupeana mikono, na kupenda tu na kila kitu ni kikamilifu. Na mwili huo unangojea kule ng'ambo. Ni sehemu yake. Ipo mitatu.

41 Unaanza Uzima wako wa Milele papa hapa madhabahuni. Hapa ndipo unapoanza Umilele. Loo! Unaanza Uzima wa Milele papa hapa. Ndipo unazaliwa mara ya pili, mwana wa Mungu. Na halafu unapokufa, unaanza … Wakati mauti yako yananakupiga katika mwili huu na moyo unakoma kupigapiga, na magurudumu yasiyodumu yanaanza kusimama kimya, kivuli hicho kidogo ambacho kilikuwa kivuli cha kivuli, katika sekunde moja kinakuwa kivuli cha kivuli, kisha kinachofuata kinakuwa kivuli, halafu kinachofuata kinakuwa kitone kidogo, halafu kinachofuata kinakuwa kijito, halafu kinachofuata kinakuwa mto, na kinachofuata kinakuwa bahari, na baada ya kitambo kidogo unakuwa umesimama mbele ya mpendwa wako wanaosimama huko ng'ambo, wamevikwa mavazi ya mwili wa kimbinguni, mpate kujuana ninyi kwa ninyi, kupendana, umegeuka kuwa kijana mwanamume na kijana mwanamke tena. Kweli kabisa. Unangojea kule hata kuja kwa Bwana Yesu. Na siku moja huo mwili Wake wa utukufu … Sasa kumbuka, huo ni mwili wa kimbinguni, si ule wa utukufu, mwili wa mbinguni. Na siku moja huo mwili wa mbinguni utaondoka Mbinguni pamoja na Yesu.

42 "Kwa maana nawaambieni," Wathesalonike wa Pili, sura ya 5, au Wathesalonike wa Kwanza, sura ya 5, mojawapo, "Nawaambieni, sitaki msijue, enyi ndugu zangu, habari zao waliolala mauti, msije mkahuzunika, kama na wengine wasio na matumaini. Kwa maana kama tunaamini Kristo alikufa akafufuka

tena siku ya tatu, vivyo hivyo wale waliolala katika Kristo Mungu atawaleta pamoja Naye. Kwa sababu twawaambieni haya kwa amri za Bwana, ya kwamba sisi tulio hai, tutakaosalia hata wakati wa kuja kwa Bwana, hatutawatangulia ama kuwazuia. Kwa maana parapanda ya Bwana italia, nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza." Miili hii ya mbinguni inashuka na kuvaa miili ya duniani, miili ya utukufu. "Na sisi tulio hai, tuliosalia, tutabadilishwa katika dakika moja, kufumba na kufumbua, kisha tutanyakuliwa pamoja nao, ili tumlaki Bwana hewani."

43 "Sitakunywa mazao ya mzabibu, au kula tena hata nitakapokula pamoja nanyi upya katika Ufalme wa Baba Yangu," ile Karamu ya Arusi. Kwa miaka mitatu na nusu yule mpinga Kristo anamaliza utawala wake, ulimwengu wote unaangamizwa, Wayahudi wanaitwa watoke, Yusufu anajijulisha kwa Mataifa, ama kwa Wayahudi. Kumbukeni, wakati Yusufu alipojitjulisha kwa ndugu zake, hapakuwapo na Mmataifa hata mmoja aliyekuwepo. Wakati alipotuma … Mnajua hiyo habari. Yusufu, mfano mkamilifu wa Kristo, katika kila hali. Na wakati Yusufu alipotuma wakaitwe ndugu zake, nao wakashuka wakaja, naye akatazama akamwona Benyamini mdogo, naye akawaona pale kisha yeye … Wakasema, "Mbona, jamaa huyu! Ha—haikutupasa kumwua ndugu yetu, Yusufu." Hao Wayahudi wanapoona ya kwamba walikuwa wamefanya kosa; sasa wakati Kristo, wakati anapojijulisha Mwenyewe kwao. Naye Yusufu alikuwa amejaa sana, ilimbidi kulia, karibu alie, kwa hiyo akamruhusu mke wake na watoto waondoke, na walinzi wote na kila kitu, na kuwapeleka katika jumba la kifalme. Kweli kabisa. Na halafu mbele za Wayahudi peke yao, akasema, "Mimi ni Yusufu, ndugu yenu. Mimi ni ndugu yenu." Na ndipo wakaanguka na kuanza kutetemeka, kasema, "Sasa tunajua tutajuta, kwa sababu tulimwua ndugu yetu. Tumesema tulimwua ndugu yetu, na sasa yeye ndiye huyu mfalme mkuu."

Yeye akasema, "Mungu alifanya hivyo kwa kusudi fulani, kuokoa maisha." Hiyo ndiyo sababu hasa Mungu alifanya hivyo, kutuokoa sisi Mataifa. Lakini Mataifa walikuwa katika jumba la mfalme. Haleluya! Akiwa amekataliwa na ndugu Zake, Yusufu, alimchukua Bibi-arusi; naye huyo Bibi-arusi alikuwa Mmataifa, si Myahudi. Vema.

44 Sasa, mnaelekea wapi sasa? Baada ya sisi kuuvaa mwili huu mtukufu, na ule wakati mkuu ujao; wakati mwili huu wa utukufu, mwili huu wa kimbinguni umefanywa mwili wa utukufu. Mnapata lile ninalomaanisha sasa? Ndipo ninaweza kutembea niende kule na kusema, "Ndugu Neville!" Hebu niwape mfano mdogo. Nasema, "Ndugu Humes, hebu na twende kwa Baba asubuhi ya leo." Yeye ni Mungu. Tunamjua sasa, Yeye ni Mwokozi, Yeye ni Mponyaji.

Kamwe hapakuwapo na kitu kama uumbaji wa dhambi. Hilo halikusikika sawa, sivyo? Dhambi si kitu kilichoumbwa. La, bwana! Dhambi ni upotovu. Kuna Muumba mmoja tu, Naye ni Mungu. Dhambi ni haki iliyopotoshwa. Uzinzi ni nini? Haki iliyopotoshwa. Uongo ni nini? Ukweli ukielezewa vibaya. Hakika. Neno la laana ni nini? Ni baraka za Mungu zilizogeuzwa kuwa neno la laana kwa Mungu, badala ya baraka. Dhambi si kitu kilichoumbwa. Dhambi ni upotovu. Kwa hiyo, Shetani asingeweza kuumba dhambi, yeye alipotosha tu kile Mungu alichokiumba. Hiyo ni kweli kabisa. Mauti ni upotovu tu wa uhai.

45 Sasa angalia jambo hili, angalia hili. Ndipo nitasogea niende kule, na nitasema, "Ndugu Humes, hebu mimi na wewe, na Ndugu Beeler na baadhi ya ndugu, tutamwendea Baba, Mungu. Na, aseme, hebu tufanye safari ndogo. Ninyi wavulana mliipenda milima mlipo …"

"Naam, hakika tuliipenda."

"Loo, kuna umbali wa hizo maili milioni kadha huko ng'ambo katika huo ulimwengu mpya. Nendeni zenu, mkazurure kule."

"Inanibidi ku …?… jua kila siku, njoni huku juu. Nitawasikia. Huku wangali wanazungumza, nitasikia." Isaya 66. Hiyo ni kweli.

46 Nanyi mnajua, ninatembea kupitia huko, sisi sote tunatembea kule kwa karibu miaka mia tano, safari ndogo tu, milioni moja, haileti tofauti yoyote, unaona. Na sasa—sasa hilo linasikika kama wenda wazimu, bali ni kweli. Unaona, ni kweli, kwa sababu hakuna wakati, ni Umilele. Na ninapoenda huko nje, nashuka natembea kupitia kule, na mnajua ni nani ni—ni—ninakutana na nani huko? Ninasema, "Vema, kama huyo si Dada Georgie Bruce! Mbona, Dada Georgie, ni muda mrefu tangu nikuone." Anaonekana tu kama vile yeye alivyo siku zote. Unaona? Huenda akawa na umri wa miaka milioni kumi, bali ni kijana tu kama alivyowahi kuwa. Yeye angekuwa akimkuna mtu fulani mgongoni, nami naangalia kule, ni duma, simba.

Nasema, "U hali gani asubuhi hii, duma?"

"Miau," kama kipaka. "Loo, nimekuwa kule chini nikizungumza na baadhi ya akina dada karibu na yale maua makubwa kule, tumekuwa kule chini yapata miaka mia tano, unaona, nikitazama huku na huko." Sasa, hilo linasikika wenda wazimu, bali ni kweli. Hilo ni kweli kabisa. Hivyo ndivyo Mungu alivyolikusudia.

47 Vema, moyo wako ubarikiwe, Dada Georgie. Hakuna madhara yanayoweza kuja, hakuna kitu kabisa. Katika wakati wa jioni tutapanda kwenye kilele cha mlima, na kusema, "Ee Baba, Mungu, wakati mmoja nilikuwa nimepotea. Loo, wakati mmoja nilikuwa katika taka za dhambi, Baba, Mungu, nawe ukaniokoa."

Mbona, watu ambao wamejaribu kueleza jambo hilo wameshikwa na wazimu. Vema, mtu yule aliyeandika ile aya ya mwisho ya ule *"Ee Upendo wa Mungu,"* ambayo ilindikwa kwenye ukuta wa hospitali ya wenda wazimu, ambaye alijaribu kuonyesha upendo wa Mungu. Jinsi alivyoinama kuwaokoa wenye dhambi, na jinsi Yeye alivyofanya, upendo Wake ulioshuka kuja kukuokoa wewe na mimi. Nena kuhusu ibada, Malaika hawajui lo lote juu yake! Kuabudu, Malaika anajua tu … Yeye husimama pale na kupigapiga mabawa Yake nyuma na mbele, na kila upande, "Haleluya! Haleluya!" Lakini, loo, rehema! Inapofikia kujua ya kwamba nilikuwa nimepotea na sasa nimepatikana, nilikuwa nimekufa, ni hai tena! Ee Mungu, nilikuwa dhambi, nilikuwa takataka, nami nilikuwa kule kwenye jalala!

48 Haya hapa yaliyo bora sana ambayo maisha yangeweza kukupa. Je! Uliwahi kushuka kwenda hapa penye jalala la Colgate? Ni mahali panaponuka sana nilipowahi kufika. Huo moshi wa kale hunichefua nikinusa harufu yake. Nikikaa kule chini katika moshi huo wote wa kale, huchefua tumbo sana, linakusokota tu, baada ya kunywa mafuta ya mnyonyo. Unaona, unachefuka sana tu uwezavyo kuwa! Na panya wakikiupitia kila mahali juu yako, wakijaribu kukula wewe. Na hayo hati ndiyo maisha bora sana. Na halafu mtu fulani ananyosha mkono wake na kukunyanyua. Nawe ni mzee sana na huwezi kujisaidia mwenyewe. Na akutwae tu na kukufanya mvulana wa miaka kumi na minane, kisha akuweke juu ya mlima, ukiwa mchangamfu sana na mwenye afya, jamani, mvuto wa pumzi nzuri ya hewa safi namna hiyo, maji mazuri ya baridi. Je! Ungelitaka kurudi kwenye jalala hilo tena? Kamwe, kamwe, kamwe, kamwe hutaenda kwenye jalala hilo tena.

49 Sasa, hiyo ndivyo inavyomaanisha, rafiki. Hivyo ndivyo lile ono, ama kuhamishwa, cho chote kile, ono. Nitasema ono, maana ninaogopa hilo lingemuudhi mtu fulani kusema kuhamishwa, hivyo ndivyo ilivyokuwa. Sasa, hapo ndipo ambapo Mungu … kile Mungu alichofanya kuleta wana na binti Kwake. Sasa, watu hawa ni akina nani? Hivi wao walipataje … Watu hawa walifanya nini kustahili jambo hili? Walipataje kufanya jambo hilo? Mungu, hapo mwanzo, kabla hata Malaika hajafanywa … Ni wangapi wanaojua Yeye hana ukomo? Kama sivyo, Yeye si Mungu. Kwa hiyo, Mungu, katika rehema Yake isiyo na ukomo, aliona ya kwamba Lusifa angefanya jambo hilo, kama Yeye aliumba hili. Yeye angewaweka kwenye uhuru wa kuamua watakalo, msingi huo. Nawe ungali pale, hiyo ni kweli, ule mti wa mema na mabaya umewekwa mbele ya kila mmoja wetu, ufanya uchaguzi wako. Naye Lusifa ndiye aliyekuwa wa kwanza kuchukua njia ya makosa. Naye akaanza kumvuta, maskini, akijaribu kuchukua yote kwa ajili yake, kujaribu kumshinda mtu fulani mwingine. Na hapo ndipo lilipoanzia. Sasa, sikilizeni jambo hili. Hapo ndipo dhambi ilipoanzia. Mungu, katika niai Yake isiyo na ukomo, aliliona hilo, na akaona njia pekee …

Sasa, ninyi ndugu wa utatu, sitaki kuwaudhi, lakinimngewezaje katika Jina la Neno zuri la Mungu kumweka Yesu kuwa mtu tofauti na Mungu Mwenyewe? Kama Yesu angeweza kumchukua mtu mwingine na kumfanya aende na kufa, ili kumkomboa mtu huyu hapa, Yeye angekuwa ni mtu asiyetenda haki. Kuna njia moja tu ambayo Mungu angeweza kufanya jambo hilo, ingekuwa kwamba Yeye Mwenyewe apachukue mahali hapo! Naye Mungu akafanyika mwili kusudi apate kuonja maumivu ya mauti, atuondolee ule mwoba na mauti, tupate kukombolewa na Yake Mwenyewe. Hiyo ndiyo sababu ataabudiwa namna hiyo. Yesu alikuwa mwanadamu, hakika alikuwa. Alikuwa mtwanadamu m-w-a-n-a-d-a-m-u, aliyezaliwa na bikira Mariamu. Lakini Roho aliyekuwa ndani Yake alikuwa Mungu bila kipimo, ndani Yake ulikaa utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili. Yeye alikuwa Yehova-yire, Yeye alikuwa Yehova-rafa, Yeye alikuwa Yehova-manase, Yeye alikuwa Yehova; Ngao yetu, Kigao chetu, Mponyaji wetu; Yeye alikuwa Alfa, Omega, Mwanzo na Mwisho; Yeye alikuwa wa Kwanza, wa Mwisho; Yeye aliyekuwako, Ambaye Yuko, Naye Atakuja; Shina na Mzao wa Daudi, ile Nyota ya Asubuhi, mbona, Yeye alikuwa Yote-katika-yote. Katika Yeye ulikaa utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili!

50 Na mauti siku zote ilikuwa na mwiba, hata iliwachoma watu, "A-ha," Ibilisi anasema, "Nimekupata, kwa sababu ulinisikiliza. Nitakuchoma, nitakuweka kaburini. Hiyo damu ya kondoo haiwezi kukusaidia chochote, hiyo ni damu ya mnyama tu." Lakini Mungu, katika hekima Yake, alijua ya kwamba kungekuwako na Mwana-Kondoo ajaye, aliyechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Naam, bwana. Nao … Yeye aliungojea wakati huo, utimilifu wa wakati utimie.

Lakini siku moja wakati huyu Mwana-Kondoo alipokuja, Mtu huyu, hata Shetani alipumbazwa. Alimwangalia Yeye kote, akasema, "Kama Wewe ni Mwana wa Mungu, fanya *hivi*. Kama Wewe ni Mwana wa Mungu, fanya muujiza na hebu nikuone ukiufanya. Hebu nikuone ukiufanya. A-ha, nitamfunga tambara usoni Mwake, nikupige. Kama Wewe ni nabii, tuambie ni nani aliyekupiga." Hum! "Mimi siamini, siamini Wewe ndiye yule Jamaa. Kama ndiwe, tuambie kinaganaga jinsi Wewe ulivyo." Unaona, yote namna hiyo. "Loo, tuambie Wewe ndiwe!" Yeye hakufungua kinywa Chake. Loo, loo, je! Yeye alimpumbaza kweli kweli wakati huo!

51 Yeye aliwageukia wanafunzi, na kusema, "Ningeweza kuzungumza na Baba Yangu na Yeye angenitumia majeshi kumi na mawili ya Malaika, kama ningetaka." Pilato hakusikia jambo hilo, unajua.

"Ikiwa Wewe ndiwe! Ukiwa ndiwe. Loo, huyo si Yeye. Mbona, mwangalie akitokwa na damu. Loo, baadhi yenu enyi askari nendeni pale na kumtemea mate usoni Mwake." Wakamtemea mate, wakamdhihaki, wakang'oa baadhi ya ndevu usoni Mwake. "Loo, Yeye siye! Naam, huyo si Yeye!

Nitamchoma kwa mwiba, jamani. Nitampata kule juu. Nimekupata sasa!"

Wakati alipolia kwa mara ya mwisho, "Eli! Eli! Mungu wangu! Mungu wangu!" Huyo alikuwa mwanadamu. "Mbona umeniacha?"

Katika bustani ya Gethsemane, ule upako ulimwacha, mwajua, ilimpasa afe kama mwenye dhambi. Yeye alikufa mwenye dhambi, unajua jambo hilo; si dhambi Zake, bali zangu na zako. Hapo ndipo upendo huo ulipoingia, jinsi Yeye alivyozichukua zangu! Loo, haleluya, jinsi alivyozichukua zangu!

52 Naye alikuwa pale, asingelifungua kinywa Chake. Mwiba ulisema, "Unajua, naamini huyo alikuwa ni mtu wa kawaida tu. Yeye hakuzaliwa na bikira, kwa kuwa nilimchoma kwa mwiba wangu."

Naye huyu hapa anakuja, akamchomeka mwiba wake, lakini huo ulikuwa wakati usiofaa, jamani! Aliacha mwiba wake ung'olewe wakati huo. Hawezi kuchoma tena tangu wakati huo, aliacha mwiba wake humo ndani. Akafufuka penye siku ya tatu, Naye akasema, "Mimi ndimi niliyekuwa nimekufa, Nami ni hai tena, Nami naishi hata milele na milele, nina funguo za mauti na kuzimu." Naam, bwana. Alishindwa kuona huyo alikuwa ni Nani. "Na kwa kwa kuwa Mimi ni hai, ninyi nanyi mtakuwa hai pia. Haijadhihirika bado …"

53 Siku moja, siku tatu ama nne baada ya hayo, baada ya Yeye kupaa kwa Baba, alikuwa amerudi, ndipo baadhi wakasema, "Loo, Yeye ni … Yeye—Yeye hana budi kuwa pepo. Yeye huyo Jamaa hana budi kuwa kitu kama mzimu. Nasi tunaninii … Mlipomwona Yeye. Mliona ono."

"La, Huyo alikuwa Yesu halisi."

Tomaso akasema, "Hebu niione mikono Yake na kila kitu, nitawaambieni kama ndivyo ilivyo."

Yeye akasema, "Mimi hapa." Kasema, "Mna samaki na mkate yo yote hapo? Nileteeni sambusa." Nao wakamletea sambusa, Naye akasimama pale na kuila. Kasema, "Sasa, je, roho hula kama ninavyokula? Je, roho ina mwili na mifupa kama nilivyo nayo?" Unaona? Yeye akasema, "Mimi Ndiye. Mimi ni huyo."

54 Naye Paulo akasema, "Haijadhihirika bado tutakuwa mwiliwa namna gani hasa, bali tunajua tutakuwa na mwili kama Wake." Ati nini? Je! Yeye alipata kuwa na mwili huo wa Kiungu? Naam, bwana! Wakati alipokufa, Biblia ilisema kwamba "Yeye," ni kiwakilishi binafsi tena, "Yeye alienda kuzimu na kuzihubiri nafsi zilizokuwa kifungoni." Haleluya! Yeye alifanyaje jambo hilo? Alikuwa na hisi za kuhisi, alikuwa na hisi za kusikia, alikuwa na hisi za kunena, alihubiri na aina ile ile ya mwili kama wa wale waliotukuzwa niliowaona hivi majuzi usiku. Yeye alizia nafsi zilizokuwa kuzimu, ambao hawakutubu katika zamani za uvumilivu wa siku za Nuhu.

Lakini wakati alipofufuka kwenye Pasaka, haikuwezekana kwamba mwili huo uone uharibifu, kwa kuwa nabii Daudi aliliona hilo hapo kabla, "Sitaiacha nafsi Yake katika kuzimu, wala sitamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu. Tena mwili Wangu utakaa katika tumaini, kwa maana hataiacha nafsi Yangu katika kuzimu, wala hatamwacha Mtakatifu Wangu aone uharibifu." Na katika masaa sabini na mawili kabla uharibifu haujaingia, huo mwili wa Kiungu, huo mwili uliokwenda na ukazihubiria nafsi zilizokuwa kifungoni, ambao hawakutubu katika uvumilivu wa siku za Nuhu, uliofufuka tena, nao wenye kufa ukavaa kutokufa, Naye akasimama na akala, Naye akatuambia ya kwamba Yeye alikuwa Mtu. Haleluya!

55 Hivyo ndivyo tutakavyomwona, Ndugu Evans. Hapo ndipo Yeye atakapoketi kwenye kiti cha enzi cha Daudi. Haleluya! Hapo ndipo tutakapotembea huku na huko sasa, nitasafiri safari pamoja nawe kuivuka milima kwa muda wa miaka milioni moja, mnaona, siku chache tu, dakika chache tu, tutavuka kule, tukaketi kule .

Na wakati wa kula unafika, mwajua, muda si muda, Dada Wood akasema … Nikasema, "Dada Wood, vema, umekuwa wapi wakati huu wote? Sijakuona kwa … inaonekana kwangu kama kwamba imepita dakika kumi na tano."

"Loo, hiyo imekuwa miaka elfu mbili iliyopita, Ndugu Branham."

"A-ha. Unajisikiaje?" Loo, bila shaka huwezi kujisikia vinginevyo ila vizuri.

"Aseme, njoni hapa, enyi wavulana, nitawaonyesha ninyi nyote kitu fulani, ndugu, ndugu zangu wapendwa. Hapa kuna chemchemi ya maji hapa, yaliyo bora sana mliyopata kunywa. Na, loo, tutakunywa maji mazuri ya baridi. Nitaunyosha mkono wangu nikachume kichala kikubwa mno cha zabibu, nasi sote tutaketi pale na kuzila." Je! jambo hilo si litakuwa zuri sana? Hivyo ndivyo ilivyo hasa. Ndivyo hasa.

56 Tulipataje hili? Tunalijuaje? Mungu, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, alituchagua tangu zamani! Akina nani? Wale walio katika Nchi ya ahadi.

> *… alitangulia kutuchagua, ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo … sawasawa na uradhi wa mapenzi yake,*

*Na usifiwe utukufu* Wake …

Ili tupate kumsifu Yeye kama alivyosema. Hivyo ndivyo alivyokuwa, Mungu. Tunataka kumsifu Yeye.

*… usifiwe utukufu wa neema yake, ambayo* ametufanyia tukubalike *katika huyo mpendwa*. Katika Kristo tumekubalika.

*Katika yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, msamaha wa* d-a-m-b-i …

57 Inanibidi kurudi kwenye kufanywa wana wenye mamlaka, lakini ninataka kukomea kwenye "dhambi" hapa kwa dakika moja. "Dhambi," mliona hilo? Unajua Mungu hamhukumu mwenye dhambi kwa kutenda dhambi? Yeye humhukumu kwa kule kuwa mwenye dhambi. Kama mwenye dhambi akivuta sigara, Yeye hamhukumu kwa jambo hilo; yeye ni mwenye dhambi, hata hivyo. Unaona? Unaona? Yeye hana dhambi zozote, mwenye dhambi hana. Yeye ni mwenye dhambi tu, unaona, hana dhambi zozote. Bali ninyi mna dhambi, ninyi ambao ni Wakristo. Unaona hapa anazungumza na Kanisa. Kulinyosha. Unaona? Unaona? "Msamaha wa dhambi," d-h-a-m-b-i. Tunafanya dhambi. Lakini mwenye dhambi ni mwenye dhambi tu, Mungu hamsamehi.

58 Sasa, unasema, "Vema, yeye alitoka hapa na kumpiga mtu risasi. Utafanya nini juu ya jambo hilo?" Hiyo si kazi yangu. Mimi si mtengenezaji, mimi ni mhubiri. Sheria itashughulikia jambo hilo, wao ni watengenezaji. Wao ni … "Vema," unasema, "yeye alifanya uzinzi." Hilo, hilo—hilo ni jukumu la sheria. Hilo ni kati yake na sheria. Mimi—mimi—mimi—mimi si mtengenezaji, siwarekebishi watu. Ninataka waongoke. Mimi ni mhubiri, unaona, kazi yangu kumpeleka kwa Mungu. Kama alitenda dhambi, hiyo ni juu yake, yeye ni mwenye dhambi. Mungu humhukumu kwa kiwango cha juu zaidi. Kwanza yeye ni mwenye dhambi, kwanza amehukumiwa. Hata hakufikia kiwango cha kwanza, yeye—yeye—yeye hayuko popote. Kwanza yeye ni mwenye dhambi. Yeye hana dhambi zozote, yeye ni mwenye dhambi.

59 Usingeweza kutoka nje na kusema, "Kiasi *hiki* ni usiku, na kiasi *hiki* si usiku." La, wote ni usiku, wote ni usiku tu. Hivyo ndivyo Mungu alivyosema. Hiyo ni kweli, yeye ni mwenye dhambi tu, kwisha. "Sasa, yeye alifanya hili, kiasi *hiki* ni usiku, *hili* ni giza angavu kweli kweli papa hapa." Ninajua, lakini lote ni giza tu, hivyo tu. Unaona?

Nisingeweza kusema, "Kiasi *hiki* ni nuru papa hapa." La, yote ni nuru tu, mnaona, nuru tu, huwezi kusema ni kiasi gani. Unaona? Lakini kama yeye ni sehemu nyeusi katika *hili*, basi kuna giza ndani yake.

60 Kwa hiyo "dhambi," d-h-a-m-b-i, tuna msamaha wa dhambi zetu kwa (nini?)Damu Yake, Damu ya thamani.

*… sawasawa wingi wa …*

Tunaisahaunamna gani? Kwa sababu tunastahili, tulifanya jambo fulani kusudi dhambi zetu zisamehewe? Ati nini Yake?

… neema;

Loo, jamani! Sina kitu mikononi mwangu ninacholeta, Bwana. Hakuna kitu ningeweza kufanya, hakuna kitu ningeweza kufanya. Tazama! Yeye alitangulia kunichagua, aliniita, alinichagua. Kamwe mimi sikumchagua Yeye. Yeye alinichagua, alikuchagua wewe, alituchagua sisi sote. Sisi hatukumchagua. Yesu alisema, "Ninyi hamkunichagua Mimi, niliwachagua ninyi." Yeye alisema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu kwanza, na wote alionipa Baba watakuja Kwangu. Na hakuna hata mmoja wao aliyepotea, isipokuwa mwana wa upotevu, kutimiza Ma—Maandiko." Mnaona? Kasema, "Lakini wote alionipa Baba watakuja Kwangu."

61 Loo, ninachelewa sana, sivyo? Nami sijatoka kwenye jambo hili bado. Bado sijaanza jambo hili. Hebu niharakishe, sina budi kufikia jambo fulani papa hapa upesi sana sasa, na tuharakishe. Sina budi kurudi kwenye huku kufanywa wana wenye mamlaka kwa dakika moja. Loo, mtanisamehe kwa—kwa dakika moja tu? Hebu na tupate hili hapa, baadhi ya watu hawa waliotoka Georgia wako hapa kwa usiku huu tu, nawatakia heri. Sasa, ndugu wa Georgia, na Texas na popote mnakotokea, sikilizeni aya hii ya 5. Hebu na tukae nayo kwa dakika chache.

*Kwa kuwa alitangulia kutuchagua ili—ili …*

62 Neno "ili" linamaanisha nini, neno "ili"? Linamaanisha kitu fulani tunachoendea, ili. "Naenda nifike kisimani. Naenda nifikie kile kiti." Humes, unalipata hilo? "Naenda nifikie kwenye lile dawati."

Sasa, Yeye *alitangulia kutuchagua, ili tufanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na uradhi wa mapenzi Yake* Mwenyewe,

Ni kiasi gani cha uradhi? Ulikuwa uradhi wa nani, wema wa nani? Wake Mwenyewe. Uradhi Wake wa Mapenzi Yake Mwenyewe!

63 Sasa, “kufanywa wana wenye mamlaka” ni nini? Sasa hebu nipate hili sasa, sijui kama … Sitakuwa na wakati wa kumaliza hili, bali nitaligusia. Ndipo kama kuna swali, mnaweza kuniuliza baadaye kidogo wakati fulani katika ujumbe, kitu fulani. Sikilizeni. Kuasili kwako kuwa mwana mwenye mamlaka si kuzaliwa kwako. Kufanywa kwako mwana mwenye mamlaka ni kuwekwa mahali pako. Wakati ulipozaliwa mara ya pili, Yohana 1:17, naamini, tunapozaliwa kwa Roho wa Mungu, sisi ni wana wa Mungu. Lakini tulichaguliwa tangu zamani. Sasa hapa ndipo ninapojaribu kuwafikisha, kwa ajili ya wana hawa wa siku za mwisho, mnaona. Ku … Unaona? Tulichaguliwa tangu zamani ku- (ili) tufanywe wana wenye mamlaka.

Sasa, sasa hebu tuendelee. Sasa, jambo hili ndilo linalowaudhi Wapentekoste kidogo. Wao wanasema, “Nimezaliwa mara ya pili! Bwana asifiwe, nina Roho Mtakatifu!” Sawa. Wewe ni mwana wa Mungu. Hiyo ni kweli. Lakini hata hivyo hilo silo ninalozungumzia. Unaona, ulichaguliwa tangu zamani upate kufanywa mwana mwenye mamlaka. Kufanywa wana wenye mamlaka, ni kumweka mwana mahali pake.

Niko karibu sana na hiyo, maana Becky aliniambia kwamba mimi huikaribia sana, hamwezi kusikia huko nyuma. Mimi nina …

64 Unaona, mtoto. Ni wangapi wanaojua sheria za kufanywa mwana mwenye mamlaka katika Agano la Kale? Bila shaka, mmeangalia. Mwana alizaliwa. Naamini nilihubiri katika mahubiri fulani. Ni upi huo, Gene, unaukumbuka? Uko kwenye kanda. Loo, ilikuwa nini? Ni—ni—ni—nimeigusia. Loo, naam, nimeupata, *Msikieni Yeye*. *Msikieni Yeye*; kufanywa wana wenye mamlaka kwa watoto.

Sasa, katika Agano la Kale, wakati m—wakati mtoto alipozaliwa katika familia, yeye alikuwa mtoto alipozaliwa, kwa sababu alizaliwa na wazazi wake, yeye alikuwa ndiye mwana wa kiume wa hiyo familia na mrithi wa vitu vyote. Sasa, lakini huyu mwana alilelewa na waalimu. Wagalatia, sura ya 5, aya ya 17 hadi ya 25. Vema. Yeye alilelewa na waalimu, walezi, waalimu. Sasa, kwa mfano, kama nilikuwa na mwana aliyezaliwa, tuseme, mimi ni baba na …

65 Na hiyo ndiyo sababu katika ile ya King James, ni wangapi waliowahi kuwazia kwamba hiyo inasome isivyo kawaida kabisa katika lile Toleo la King James, kasema, “Katika nyumba ya Baba Yangu mna majumba mengi”? Nyumba, majumba mengi. Unaona? Kwa kweli, katika—katika siku ambazo Biblia ilifasiriwa kwa ajili ya Mfalme James, *nyumba* ilikuwa ni “milki.” “Katika *milki* ya Baba Yangu mna majumba mengi.” Si katika nyumba, majumba ya kifahari, bali aliitwa Baba wa milki hii. Walikuwa nayo Kibiblia kabisa, katika Biblia hivyo ndivyo ilivyo.

Wakati baba alipokuwa na shamba kubwa mno la ekari elfu moja, ama kitu kinginecho, alikuwa na kundi la watu wanaoishi *hapa*. Alikuwa amewaajiri wafanyakazi walioishi *humu* kuwachunga kondoo, alikuwa na wengine *hapa* kuwachunga ng'ombe, alikuwa na wengine *hapa* ambao walikwenda kwenye nyanda za juu kule umbali wa maili mia moja, na alikuwa na wengine papa *hapa* wawachunga mbuzi, na alikuwa na wengine waliochunga nyumbu na—na vitu mbalimbali. Yeye—yeye alikuwa tu na ufalme mkubwa. Naye akampanda maskini punda wake na akamzungukia kila mmoja na kuona jinsi walivyokuwa wakiendelea, ukataji wa manyoya ya kondoo na kila kitu namna hiyo. Hakuwa na wakati …

Hamwezi kunisikia ninapoondoka pale. Ni—ni—nitajaribu kukaa hapa nyuma. Mnaweza kunisikia vizuri sasa hivi, hapa? Tazamaneni.

66 Akamwendesha punda wake, na akaenda zake, ku-kushughulikia ufalme wa-wa-wake. Kwa hiyo sasa anataka … Huyo mwana atakuwa mrithi wa kila kitu alicho nacho. Yeye ni mrithi.

Na wakati tunapozaliwa katika Ufalme wa Mungu, na Yesu Kristo, sisi ni warithi wa Mbinguni, warithi pamoja na Yesu, kwa sababu Yeye alipachukua mahali petu. Yeye alifanyika sisi (dhambi), tupate kuwa Yeye (haki). Unaona? Yeye alifanyika mimi ili nipate kuwa Yeye, mnaona, warithi pamoja Naye. Vema, sasa kumbukeni jambo hilo, kwa kila mmoja wenu.

67 Sasa, kumbuka, Mungu alitangulia kukuchagua, kwa kujua tangu zamani, kwamba ulikuwa ukifikia jambo Hili. Kila mtu anayeelewa hilo, inua mkono wako juu, unaona. Mungu, kwa kutangulia kujua, alikuchagua tangu zamani kuja kwenye Nchi ya ahadi. Nchi ya ahadi ni nini kwa Mkristo leo? Inua tu mkono wako juu kama unajua. “Ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu, kwa hao walio mbali. Na itakuwa katika siku za mwisho, asema Mungu, kwamba nitaimwagia Roho Yangu juu ya wote wenye mwili, wana wenu na binti zenu.” Na katika Isaya 28:18, “Amri juu ya amri, kanuni juu ya kanuni; hapa kidogo, pale kidogo. Shikilia yaliyo mema. Kwa kuwa kwa lugha nyingine na kwa midomo ya watu wagemi nitasema na watu hawa. Na huku ndiko kuburudika, (ile—ile Raha) ile nchi ya sabato niliyosema wanapaswa kuingia. Na, kwa haya yote, hawangesikia, bali walivitikisa vichwa vyao na kuondoka, wala hawakutaka kulisikia.” Unaona? Kweli kabisa.

68 Ilikuwa ni kitu gani? Ni kama tu wale watu waliokuwa waliopanda kutoka Kanaani, ama kutoka Misri, wakaja kote kupitia jangwani, nao wakafika karibu kabisa, karibu vya kutosha kuonja zabibu zilizotoka kwenye ile nchi. Ndugu, kule, hao watu wananitaka nighairi hayo, hayo yaliyomo kwenye Waebrania 6.

Ninawezaje kufanya jambo hilo? Hao ni waamini wakwamia mpakani, kamwe hawatavuka! Hawawezi kuvuka. Yesu alisema.

Wao wasema, "Baba zetu walikula mana jangwani."

Naye Yesu akasema, "Hao, kila mmoja wao, amekufa." Hcho ndicho kilichowatenganisha. Hao, kila mmoja wao, amekufa. Hiyo ni kweli. Kasema, "Bali Mimi Ndimi Chakula cha Uzima kitokacho kwa Mungu Mbinguni. Mtu alaye Chakula hiki, hatakufa kamwe. Hiyo ni kweli. Naam, bwana, yeye anao Uzima wa Milele kama akila Hiki, Mimi Ndimi ule Mti wa Uzima tokea bustani ya Edeni."

69 Sasa, unaona, watu hawa wanakuja karibu sana! Unaona, kama ukiangalia katika Waebrania 6, siyo kuyarudai hayo, bali katika Waebrania 6, "Watu hawa wakiisha kufanywa washirika, wanakaribia sana, na wameonja kipawa cha Mbinguni." Waliketi humu, wakaona uponyaji ukifanyika, wakaona watu katika nguvu za Mungu, wakaona maisha yakibadilishwa, bali hawataunga Hayo mkono. La, bwana. La, bwana. "Nao nimeonja nguvu za ulimwengu ujao; na kama wao wakijaribu kujifanya upya wakatubu, kwa kuwa—kwa kuwa wamemsulibisha Mwana wa Mungu upya upya, na kuihesabu Damu ya agano ambayo kwayo walitakaswa …"

"Mimi ni mfuasi wa kanisa linaloamini katika utakaso." Lenyewe hilo ni sawa, bali husongi mbele vya kutosha. Unaona? Naam, bwana. Jangwa liliwatakasa. Naam, hakika. Wao walikuwa na—walikuwa na nyoka wa shaba na ma—madhabahu ya shaba, na kila kitu huko nje, utakaso, bali waliingia Palestina kwa ajili ya raha. Hawaku …

70 Angalia katika Waebrania 4, je, yeye hakuisema "Raha nyingine"? Mungu aliumba siku ya saba na akawapa raha siku ya saba. Mahali pengine alinena juu ya siku ya pumziko, "na leo katika Daudi." Kisha akawapa Pumziko lingine, "Njoni Kwangu ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nitawapa Pumziko." Ingieni katika hili Pumziko! Kwa maana sisi ambao tumeingia katika hili Pumziko tumestarehe wenyewe kutoka katika kazi zetu kama vile Mungu alivyopumzika kutoka katika Zake kwenye sabato. Hakika. Hiyo hapo sabato yako, Pumziko. Hilo hapo ndilo Pumziko lako halisi katika Nchi hii ya ahadi.

Roho Mtakatifu ni ahadi ya watu. Na kwa nini wawatake wahubiri wenye elimu ambao watawaacha wavae kaptura na kukata nywele zao, na kujipaka rangi mdomoni, na watu wanaocheza kamari na kunywa bia na kufanya mizaha, na kuendelea na kuendelea namna hiyo, na kujiita wenyewe washiriki wa kanisa? Mbona, watachukua kitu kama hicho na kukataa uongozi wa Roho Mtakatifu! Mbona, Biblia ilisema Neno la Mungu ni kali kuliko upanga wenye makali kuwili linalokata na kutenganisha mifupa, na hata huyatambua mawazo ya moyo. Naam, hata mawazo ya nia!

71 Na kama tukiupenda ulimwengu au mambo ya ulimwengu, hata upendo wa Mungu haumo ndani yetu. "Waitwao ni wengi, wateule ni wachache; kwa maana mlango ni mwembamba na njia imesonga iongozayo Uzimani, na ni wachache watakaoiona. Wengi watakuja Kwangu katika siku hiyo na kuketi katika ule Ufalme," alisema Yesu,"pamoja na Ibrahimu, Isaka na Yakobo. Lakini wana wa ufalme watatupwa nje, na waseme, 'Bwana, hatukufanya hivi katika Jina Lako? Hatukuhubiri? Hatukuwa Daktari *Fulani* na Kasisi *Fulani*?' Sikuwajua kamwe. Ondokeni Kwangu, enyi mtendao maovu, sikuwajua. Si wote wasemao, 'Bwana, Bwana,' watakaoingia. Bali ni yule atendaye Mapenzi ya Baba Yangu aliye Mbinguni, huyo ndiye anayeingia."

72 Haya basi, kuingia katika Nchi hii ya ahadi. Tunaingiaje? Tumechaguliwa tangu zamani kuiingia hiyo. Kanisa, kwa kujua kwa Mungu zamani, limechaguliwa tangu zamani (kwa ajili gani?) Kwa ajili ya heshima Yake, kwa neema Yake, kwa utukufu, na ibada na utukufu wa Mungu. Baba, akiwa ameketi kule nyuma mwanzoni, anayeishi peke Yake, hakuna kitu kilichomzunguka, alitaka kitu fulani cha kuabudu, kwa hiyo Yeye alitangulia kulitenga na kulichagua kanisa tangu zamani, na kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, na kuweka majina yao katika Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, wakati wao … aliyechinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, wapate kuonekana kwa ajili ya utukufu Wake na kwa sifa Zake mwishoni mwa wakati, wakati Yeye atakapovikusanya vitu vyote katika huyo Mtu mmoja, Kristo Yesu. Whiu! Utukufu! Hivyo ndivyo ilivyo. Hiyo ni ninii tu … Nayo ndivyo hiyo papo hapo, ndugu yangu, dada. Uje kamwe ukatoka kwenye Hilo.

73 Mungu, kwa neema Yake ya kuchagua, alikuita. Mungu, kwa neema Yake ya kuchagua, alikutakasa. Mungu, kwa neema Yake ya kuchagua na nguvu Zake, alikubatiza na kukuweka katika nchi hii ya Pumziko. Wale ambao wameingia katika Pumziko hili wameachana na kupotoka kwao. Wamestarehe wenyewe mbali mbali na kazi zao kama vile Mungu alivyostarehe kutoka kwenye kazi Zake. Wana furaha isiyoneneka, na wamejaa utukufu! Mti wa Uzima unachanua ndani yao. Wao wana uvumilivu, upole, wema, saburi iletwayo na imani, imani, upole, unyenyekevu, na kadhalika. Mti wa Uzima unachanua ndani yao kwa sababu tumaini lao limetiwa nanga katika Kristo Yesu, ushahidi wa Roho Mtakatifu ukishuhudia kwa ishara na maajabu vikiwafuata waaminio. "Ishara hizi zitawafuata hao waaminio." Wanaposonga mbele, wanawaponya wagonjwa, wanafukuza mapepo, wananena kwa lugha, wanaona maono. Wao … Nao wanatembea pamoja na Mungu, wanazungumza na Mungu. Hakuna ibilisi anayeweza kuwatikisa, wao ni imara, wakitafuta …?… Wakiyasahau hayo mambo yaliyopita, wanakaza mwendo waifikilie ile mede ya

mwito mkuu katika Kristo Yesu. Hao hapo. Hao hapo. Hilo ndilo Kanisa.

74 Walifikaje mle? Huwezi kusema, "Vema, Bwana, unajua, siku moja nilianza kuvuta sigara, nami nikaanguka, ndipo nikafikiri ninge- …" Loo, la, la, la, la.

Kuchaguliwa tangu zamani! Yeye alituita na tulipomfuata ndipo tunaposema, "Mungu, tulikuwa tumepotea na kuharibika. Hata hatukufikiria kujiokoa sisi wenyewe. Tulikuwa na asili ya nguruwe, kwanza tulikuwa nguruwe."

Hebu nenda kwenye zizi la nguruwe na kumtazama maskini nguruwe jike mzee, na useme, "Sasa, tazama hapa, maskini kipenzi, nataka kukuambia jambo fulani. Ni kosa kwako kunywa maji machafu."

Yeye angesema, "Oink-oink." Unaona? Sasa, hiyo ni kama tu usivyoweza kujiokoa mwenyewe. Hiyo ni kweli kabisa.

75 Unasema, "Bibiye, haikupasi kuvaa nguo namna hiyo, unapaswa kuvaa vizuri. Unapaswa kufanya *hivi*. Haikupasi kwenda kwenye … Haikupasi kuwa na karamu hizi za kadi. Haikupasi kuvuta sigara. Haikupasi kufanya *hivi*. Bwana, haikupasi kubeba *hcho*."

Yeye anasema, "Oink-oink. Mimi ni mfuasi wa Oink-oink." A-ha. "Oink," hilo tu ndilo wanalojua. "Vema, nataka ujue kwamba mimi ni mzuri tu kama ulivyo wewe. Oink-oink!" Unaona, wao wanakataa uongozi wa Roho Mtakatifu, kwa kuwa Biblia ilisema kwamba ukiupenda ulimwengu au mambo ya ulimwengu, upendo wa Mungu hata haumo ndani yako.

76 Nini kinachowafanya kuwa wa kipekee? Ninyi ni taifa takatifu. Mmefanya nini? Mmeingia kutoka nchi ile. Mko katika Nchi nyingine. Mliingiaje mle? Hiyo ndiyo Nchi ya ahadi. Ahadi ya namna gani? "Itakuwa katika siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwaga watu wote Roho Yangu." Kwa Roho mmoja sisi sote tumebatizwa katika Nchi hii moja ya ahadi. Amina. Ndugu na dada, haleluya, kwa usafi wa moyo, bila wivu, bila uadui, bila chochote! Sijali kama ndugu anapotea, haidhuru anafanya nini, utaondoka uende ukamtafute.

77 Nilimwendea ndugu fulani si muda mrefu uliopita, alikuwa amepotea. Kijana mmoja akaniambia, kasema, "Achana na huyo mhuni. Achana naye."

Nikasema, "Kama nikifikia mahali ambapo moyo wangu haumpendi ndugu yangu, basi ni wakati wangu wa kwenda madhabahuni, kwa sababu nimeanguka kutoka kwenye neema." Nikasema, "Nitamwendea mradi tu ana pumzi mwilini mwake, nami nitampata mahali fulani njiani." Naam, bwana. Nami nikampata, haleluya, nikamrudisha. Naam, bwana. Yeye amerudi kwenye kundi na yu salama sasa. Naam, bwana. Yeye angalikuwa amepotea bila shaka.

78 Muda mfupi uliopita nilipomwona maskini mwanamke huyo ameketi pale, na yule liwali akaniita, kasema, "Mbona, anapaswa kuvalishwa vazi la wenda wazimu." Kasema, "Anapayukapayuka tu, amerukwa na akili." Yeye—yeye, walimweka katika hoteli. Wakaja. Nikasema, "Hilo ni sawa."

Kasema, liwali akasema, "Mbona, Billy!" Mimi namjua vizuri sana, na nilimjua tangu nilipokuwa mtoto mdogo. Akasema, "Kama kuna jambo lolote ninaloweza kufanya kukusaidia."

Nikasema, "Hilo ni sawa."

Kasema, "Unaweza kumsaidia huyo mwanamke?"

Nikasema, "La, bali *Yeye* anaweza." Nikasema, "Hebu kidogo."

Kwa hiyo wakamleta kule. Na wakati alipoondoka muda mfupi uliopita, kwa amani. Ilikuwa ni kitu gani? Tulituma maombi yamfuate. Amina! Alikuwa ninii hasa…

Wao wakasema, "Je! Unataka daktari?" Wakamwambia mumewe, "Je! Unataka daktari?"

Kasema, "Daktari hawezi kumsaidia." Na hiyo ni kweli. Yeye ana kichaa; daktari hawezi kumsaidia.

Kasema, "Tumaini letu pekee ni kufika *kule*."

Naye akasema, "Billy, sielewi jambo hilo."

Nikasema, "Sitarajii wewe uelewe, unaona. Sikutarajii uelewe."

79 Lakini, loo, jamani, wala mimi silielewi! La. Lakini, ndugu, Mungu Mbinguni … Nilikuwa mbali, huko mbali wakati mmoja, Kitu fulani kikanifuata. Amina! Si kwamba nilitaka kuja, lakini, la, Kitu fulani kilinifuata. Kwa sababu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, Mungu alitangulia kuchagua, haleluya, kwamba sisi tungekuwa Wake, kwa ajili ya heshima na utukufu Wake. Sikilizeni! Wale aliotangulia kuwajua, amewafanyaje? Kawaita. Hiyo ni kweli? Je, Yeye alikuita? Naam! Kwa nini alikuita? Yeye alikujua tangu zamani. Wale aliowajua tangu zamani, aliwaita; hao ambao aliwaita, amewahesabia haki. Hiyo ni kweli?

Na hao aliowahesabia haki, amewatukuza! Amina! Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema. Hao aliowajua tangu zamani, aliwaita. Kila kizazi! Hao aliowaita, tayari amewatukuza. Nini? Hebu nisome Maandiko hapa. Vema.

> *Kwa kuwa alitangulia* kuwachagua, *ili wafanywe wanawe kwa njia ya Yesu Kristo, sawasawa na mapenzi* Yake Mwenyewe …
>
> Kwa sifa za utukufu Wake …

Loo, mnalipata hilo? Kwa sifa za utukufu Wake! Kwamba Yeye angeweza kuketi hapo katika nyakati za Milele zijazo, na watoto Wake wangepaza sauti, "Abba, Baba! Abba, Baba!"

Nao Malaika wanasema, "Wanazungumzia nini? Wanazungumzia nini?"

80 Imeonyeshwa vizuri sana katika mwana mpotevu. "Nilikuwa nimepotea." "Huyu ni mwanangu. Alikuwa amepotea na sasa amepatikana. Alikuwa amekufa, naye yu hai tena. Mleteni ndama aliyenona, joho bora zaidi, pete na mkaitie kwenye kidole chake. Na hebu tu sisi …" Si ajabu wakati nyota za asubuhi zilipoimba pamoja, wana wa Mungu walipaza sauti kwa furaha, walipouona mpango wa wokovu, Mungu akiliweka jina lako kwenye Kitabu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.

81 Sasa unasema, "Calvin aliamini kitu kama hicho." Mimi sikumwamini Calvin. Calvin alikuwa mwuaji. Calvin alimwua mtu kwa sababu alibatiza katika Jina la Yesu. Yeye alikuwa mlaghai, alihitaji kuongoka, yeye binafsi. Naam, bwana. Lakini yale aliyosema, kuhusu baadhi ya mambo aliyosema, alikuwa sahihi. Msininii … bali yale yeye … Matendo yake, mtu anayemwua mtu kwa jambo kama hilo, ni la kutisha, hiyo ni dhambi. Vema.

> *Ambayo ametuneemesha* kwetu sisi …

82 Loo, ngoja, sikupata kule "kufanywa wana wenye mamlaka," sivyo? Nimechelewa sana? Hebu tuone kile saa hii inachosema hapa, wakati tulio nao. Vema. Hebu—hebu na tuchukue dakika kumi kwa ajili ya watu hawa ambao wametoka mbali sana. Tazama. Tazama.

83 "Kufanywa wana wenye mamlaka," hebu niwaonyeshe ni kwa nini inafanywa sasa. Baba ana ufalme mkubwa, yeye anauzunguka. Sasa mwana anazaliwa kwake. Loo, yeye yuna furaha sana! (Huyo ni Mungu.) Kwa hiyo unajua kile huyo baba anafanya? Yeye anamtafuta mleaji aliye bora sana, mwalimu. Mnajua mwalimu ni nini, sivyo? Ni mwalimu wa shule. Anamtafuta mwalimu bora sana wa shule anayeweza kumpata nchini kote. (Na ndipo tunaenda sasa, sikilizeni.) Naye anamtafuta mwalimu bora wa shule anayeweza kumpata. Yeye hamtafuti tu aliye mlaghai, anataka mvulana wake awe mtu hasa.

Hivi hamtaki watoto wenu wawe hivyo? Hakika, kilicho bora mwezavyo kuwapa! Naam, bwana. Kwa hiyo kama mtu wa kawaida aliwazia jambo hilo, unafikiri Mungu anawazia nini juu ya watoto Wake? Kilicho bora sana ambacho angeweza kupata.

84 Kwa hiyo, yeye anataka mtu ambaye atakuwa mwaminifu. Sasa, yeye hataki … hataki mtu wa kusema, "Sasa, angalia, ni—ni … Kadogoo, wewe fanya tu lo lote unalotaka kufanya, mpenzi." "Loo, naam, baba, a-ha, anaendelea vizuri, yeye ni mvulana mzuri." Anampigapiga kidogo mgongoni mwake na kumpongeza. La, la. Jamaa huyo angefukuzwa kazi sasa hivi. Hakika. Anataka mtu atakayekuwa mkweli. Kama mvulana huyo anakua vizuri, anamwambia. Kama hakui vizuri, anamwambia shida yake.

Na kama baba wa duniani aliwaza hayo … Hivi hungetaka mtu awe mwaminifu kwako, mwalimu wa shule awe mwaminifu juu ya watoto wako? Hakika. Vema, unafikiri Mungu anawazia nini? Naye anajua; sisi hatujui, Yeye anajua. Sisi tuna kikomo, tusingeweza kujua. Lakini Yeye hana kikomo na anajua.

85 Kwa hiyo, unajua kile Baba alichofanya? Yeye kamwe hakusema, "Nitamtafuta papa fulani awe mlinzi wa watoto Wangu." Wala Yeye hakusema, "Nitamtafuta a—askofu." La, la. Yeye hakufanya hivyo, maana alijua papa angekosea, vivyo hivyo na askofu pia. Unaona? Yeye kamwe hakusema, "Nitamtafuta mwangalizi mkuu ayatunze makanisa Yangu." La, la.

Yeye alipamta Roho Mtakatifu. Huyo ndiye aliyekuwa Mwalimu Wake, a-ha, kuwalea watoto Wake. Vema. Basi ungejuaje kwamba Roho Mtakatifu anajua jambo hilo? Yeye hunena kupitia midomo ya mwanadamu. Unajuaje basi Yeye anasema Kweli? Unapomwona Roho Mtakatifu akinena kupitia midomo inayosema Kweli kabisa kila wakati, akibashiri na yanatimia kikamilifu kabisa, kama Samweli alivyosema, basi ujue hiyo ni Kweli. Hilo linatimia. Kwa sababu Mungu alisema, "Kama akinena na asemalo halitimii, msimsikie, maana Mimi siko pamoja naye. Lakini iwapo yatatimia, vema, basi msikieni, maana Mimi niko pamoja naye." Unaona? Haya basi. Hivyo ndivyo Yeye anavyofanya.

86 Sasa, ndipo Yeye anazunguka. Sasa, unafikiri huyo Mwalimu angesema nini kama ilingembidi kwenda kwa Baba? Na kusema, "Watoto Wa-Wako wanatenda vibaya sana. Nakwambia, huyo mvulana Wako, yeye, loo, ni mhuni. Yeye hana ujuzi wa kazi, sijapata kuona jamaa kama huyo! Jamani, unajua analofanya? Na huyo msichana Wako! Loo, whiu, sijui utafanya nini na huyo msichana. Hmm. Vema,

unajua nini? Anaonekana vile tu kama … Yeye amejipodoa kwelikweli kama baadhi ya hao wasichana huko nje. Mfilisti. Naam, Bwana, yeye anataka kutenda tu kama wanavyotenda.”

“Ati Binti yangu?”

“Naam, binti Yako.” Hao ndiyo Roho Mtakatifu anavyosema kuhusu kanisa leo. Si ajabu hatuwezi kuwa na uamsho. Unaona? Sasa, hiyo ni kweli.

“Vipi kuhusu mwanao? A-ha? Jambo lile lile.”

“Ati nini?”

87 “Vema, unajua Wewe daima ulisema ya kwamba kondoo hao wanapaswa kulishwa kwenye yale malisho kule kwenye hicho Chakula cha kondoo kule. Naam, unajua alilofanya nini? Aliwateremsha akawaingiza kwenye lundo hilo la magugu. Aliwateremsha wote tu kule chini kwenye lle ghuba ndogo, na kuwaacha wakae kwenye hilo lundo la magugu, wakila hayo majani ya kale ya miti, nao wamekonda sana ni vigumu sana kwao kutoka humo.” Hao ni maaskofu, wachungaji wanaokataa Nguvu zake. “Vema, nakwambia kweli, sijawahi kuona kundi la kondoo lenye wasiwasi kama hilo maishani Mwangu.” Yeye hapendi jambo hilo. La. “Nawe unajua? Hao ng'ombe hapa juu, Wewe unajua uli—uliwaambia wale hayo—hayo majani ya alfalfa pale, unajua, ili wanenepe?”

“Naam.”

“Unajua anachowalisha?”

“La.”

“Hayo magugu magumu. Naam. Yeye anawafanya wajiunge na mashirika na kila kitu. Hujawahi kuona kitu kama hicho maishani Mwako. Hujawahi kuona kitu kama hicho katika maisha Yako yote. Unajua analofanya? Anatoka kwenda huku na huko akivuta sigara kubwa, kifua mbele. Ameambatana na mke wake, huyo amevaa kaptura kama tu vile Wafilisti wanavyofanya kule. Naam.” Huo ndio aina ya ujumbe ambao Roho mtakatifu analazimika kupeleka kuhusu kanisa leo. Sasa, unaonaje kuhusu jambo hilo?

Huko ndiko kufanywa wana wenye mamlaka. Yeye ali … alifanya nini? Yeye alitangulia kutuchagua—sisi tupate kufanywa wana wenye mamlaka. Yeye alitupa Roho Mtakatifu; lakini, ngoja kidogo, kufanywa wana wenye mamlaka, hilo ndilo tunalozungumzia. Kufanywa wana wenye mamlaka!

88 “Vema, Wewe unajua analofanya? Askofu alikuja hivi majuzi, na kumwambia. Alikuwa akifanya ibada ndogo ya uponyaji kule, naye askofu akaja pale. Jamaa fulani, ndugu mmoja akaja na alikuwa akiwaombea wagonjwa. Naye akasema, 'Acha jambo hilo!'

“'Loo, loo, ndiyo, baba askofu, nitafanya hivyo.'

“Usishirikiane nao.'

“'Loo, la, la, baba askofu, bila shaka sitafanya hivyo.'

“Nami hapa nakuja na kumwambia Kweli moja kwa moja kutoka kwenye Neno Lako. Unaona, Hili hapa. Nilimsomea sheria Zako jinsi ya kufanya hasa, naye hangezisikiliza. Alisema, 'Loo, hilo lilikuwa kwa ajili ya wakati mwingine, mwana mwingine wakati mwingine. Hilo halimaanishi kwamba ni mimi.'” Haya basi. Hiyo, sasa hiyo ni Kweli, rafiki. Sasa hamwoni pale kanisa linakosa kuwekwa mahali pake, kwa nini hatuna uamsho, kwa nini mambo yetu hayasongi mbele? Hapo ndipo jambo lilipo.

89 Yoshua alisema, “Gadi, nawataka ninyi mu … papa hapa ndipo mahali penu kulingana na ile ramani, mahali penu pako hapa, papa hapa. Ingieni humu, Gadi, na mkae hapa. Benyamini, ninyi shukeni mwende huku moja kwa moja. Na sasa ninyi nyote msiukaribie mpaka wa Wafilisti.” Naye Yoshua anarudi, nao wote wako kila mahali kwa Wafilisti, wakifanya yale makelele mengi ya kale, wakicheza tu namna hiyo, nao wanawake wote wakijipodoa, na wakicheza huko na huko wakifurahi na kufanya anasa. Naye Yoshua anajikuna kichwa chake, na kusema, “Sasa nini?” Sasa hilo ndilo hasa linalotukia; si wote, Mungu ashukuriwe, si wote, bali ni wengi mno. Vema.

90 Sasa ni nini kinachotendeka basi? Hilo ndilo lililotukia. Hivi hawazii Mtu huyo, Roho Mtakatifu, huiva uso mbele za Baba inapomlazimu kusema hayo? Loo, jamani! “Ni—ni—nilimwambia, lakini ha—ha—yeye hangelisikiliza Hilo. Nilimwambia jambo hilo, na nikamwacha asome humo humo katika kile Kitabu. Nilikuwa—nilikuwa nimemletea mhudumu mmoja mdogo na kumwonyesha ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Nawe unajua nini? Yeye alimwachilia mmoja wa haoo—alimwachilia mmoja wa hao wachunga mbuzi aje hapa na kumwambia ya kwamba hayo yalikuwa kwa ajili ya kipindi kingine. Unaona? Naye alinuka mbaya sana wakati alipofika kule, kwa harufu ya mbuzi, Unajua, sigara, na Wewe unajua, na kadhalika, alinuka vibaya sana alipofika hapa. Unaona? Lakini nawaambia, huyo mchunga mbuzi alikuwa ametuzwa nishani za kutosha, kwa kuwa, nakwambia, kama ungeandika jina lake katika

gazeti, ingechukua (tanzia yake) ingechukua nusu ukurasa kuandika vyeo vyake. Naam, Bwana, hakika wao wanampenda kule katika nchi ile, lakini, nakwambia, hakika yeye hajui jinsi ya kuwalisha kondoo. Hilo ndilo jambo moja kwake. Yeye hatanisikiliza Mimi," asema Roho Mtakatifu. "Nilijaribu kumwambia kwamba Wewe ni yeye yule jana, leo, na hata milele, bali yeye—yeye hangesikiliza. Yeye ndiye mwoga mkuu sana niliyepata kuona maishani Mwangu. Naam. Na kanisa limemfanya mwangalizi, askofu, kadhalika, watu wote wanamsikiliza. Na halafu unajua nini? Wanachukua hizo … wana kitu kidogo cha kale kule wanachokiita 'televisheni.' Unazungusha kidude kidogo cha kale namna hiyo, na—na hao wanawake wanajitokeza na kufanya yasiyofaa, mavazi ya kila aina ya kuwa nusu uchi. Na, Unajua, wengi wa binti Zako wana- …"

"Loo, la hasha!" Unaona?

91 Kasema, "Naam, wanashiriki. Ndiyo, wanafanya hivyo. Hum. Baadhi yao wanalilia uamsho, Baba, baadhi yao wanautaka hasa. Baadhi yao kweli wanatembea ipasavyo, baadhi yao wanasimama kwa uaminifu kabisa kwenye hilo Neno wawezavyo kuwa. Wengine, sijui la kufanya, wako—wako huko nje kabisa. Unajua kile hao wengine wanachofanya? Wanawadhihaki, wakisema, 'Hao ni kundi la wenda wazimu tu.'"

"Vema, hilo linanifanya Mimi nijisikie vibaya sana."

92 Lakini sasa hebu tubadilishe hiyo picha. Sasa Baba, mwanawe ni mvulana mzuri. Baba Yake tangu—tangu mwanzo, huyu hapa Mwalimu, Roho Mtakatifu. Ni njia gani Roho Mtakatifu, Yeye alisema, "Nitatembea," yule Mwalimu alisema, "Mimi ni …"

Yule mtoto akasema, "Nitatembea moja kwa moja na Wewe. Nitaambatana Nawe moja kwa moja."

"Loo, kilima ni kirefu sana, mwanangu."

"Nitaambatana nawe moja kwa moja. Nina imani Kwako. Kama nikianza kuchoka, Yeye atauinua mkono wangu juu na kunishikilia."

"Lakini kuna simba huko kilimani!"

"Haijalishi mradi tu Wewe uko karibu, haileti tofauti hata kidogo. Ninatembea moja kwa moja pamoja na Wewe."

"Kuna tatizo huko juu, ni miamba inayoteleza."

"Sijali mimi, mradi tu Wewe umenishika mkono, nitatembea moja kwa moja na Wewe. Nitatembea moja kwa moja na Wewe."

"Loo, unajua nini? Baba Yako alikuwa akifanya hivyo, unaona. Hilo ni zuri. Naam, bwana."

93 Kapanda juu ya kile kilele cha kile kilima. "Loo," Yeye akasema, "Je, unajua nini, Baba? Mwanao ni kama tu kipande kilichotolewa kwenye lile gogo pale. Yeye ni kama Wewe kabisa, kabisa. Kila Neno unalosema, yeye analiitikia kwa 'amina.' Ni—nilimfanya aifungue katika Biblia hivi majuzi, Nayo ikasema, 'Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.' Unajua alilosema? Alipaza sauti na kuitupa mikono yake juu hewani, na kusema, 'Haleluya! Amina!' Loo! Na unajua ilisema hapa, katika—katika Neno Lako, unajua, pale Wewe uliposema, 'Zile kazi, yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya'?"

"Naam, nakumbuka kumwandikia Mwanangu Hayo. Naam, nakumbuka kuandika Hayo."

"Loo, alipoona hilo, alipaza tu sauti na kurukaruka, akipiga kelele, 'Haleluya, bwana Uondoe ulimwengu wote ndani yangu. Nifanye namna Hiyo! ' Naam, Bwana. Na mambo hayo yote aliyofanya!"

"Loo," Baba akasema hilo, "Ni—nina furaha kwa ajili ya huyo mwana. Huyo ni mwana mwema. Vema. Mwangalie kwa miaka michache, uone jinsi yeye—uone jinsi atakavyojimudu, na jinsi anavyoendelea." Baada ya kitambo kidogo miaka ikapita. "Anaendeleaje?"

94 "Loo, jamani, hata anakua katika neema! Loo, jamani! Yeye ni ninii tu … Yeye anabambua miti. Nakuambia, yeye—yeye kweli … Mbona, yeye huwachukua hao kondoo, anaweza kuwachungakama—kama tu Wewe unavyofanya. Kamwe yeye hatawapa magugu ya baharini. Kamwe hatawapa magugu magumu. Wanapomkaribia, wakisema 'tunataka kujiunga na kanisa'; yeye anasema, 'Nyamazeni, hamhitaji hilo! La, bwana. Haya ndiyo mnayohitaji, "Tubuni mkabatizwe, kila mmoja wenu, katika Jina Lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu. Mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu."' Naam, Bwana, hilo ndilo alilosema."

"Loo, kweli yeye anasema hivyo?"

"Naam, Bwana, hakika anasema Hivyo."

"Vema, hivyo ndivyo tu nilivyoliandika."

"Hivyo ndivyo anavyolisema Hilo."

"Hmm!" Naam, Bwana.

95 "Baadhi yao walisema, 'Kaeni katika mji wa Yerusalemu hata mtakapovikwa nguvu zitokazo Juu. Kwa kuwa Roho Mtakatifu amekuja juu yenu, mwe mashahidi Wangu katika Yerusalemu, Uyahudi na Samaria, na kwenye ncha za ulimwengu.' Wakati aliposoma hayo, alipaza sauti, 'Haleluya, hilo ndilo unalohitaji!' Mnajua analofanya? Yeye huwapeleka tu moja kwa moja kule mpaka wanalifahamu Hilo, hivyo tu, anakaa moja kwa moja pamoja nao.

"Na kama wakianza kuzozana, yeye anasema, 'Basi, basi, basi, hebu kidogo, hebu kidogo. Hivyo ndivyo mbuzi wanavyotenda, si kondoo. Unaona? Mnaona?' Loo, wakati mwingine wao humkasirikia kidogo, lakini yeye kwa namna fulani huwapigapiga mgongoni kidogo, aseme, 'Hebu kidogo, shsh, sh-sh, sh. Sawa.' Yeye kweli anajua jinsi ya kuwaongoza hao kondoo. Naam, Bwana, nakwambia.

96 "Je, unajua? Nilimwona Askofu Mkuu *Fulani* akimwambia ya kwamba 'hangeweza kuja katika mji huu na kufanya mkutano.' Lakini, Unajua, kwa namna fulani nilimwongoza, nikasema, 'Nenda hata hivyo.' Unaona? 'Rudisha kanda hizi, wala usiziruhusu zisambazwe.' Tulienda hata hivyo! Tulikwenda katika miji hii hapa, kasema, 'Vema, hatutadhamini- …'

"Nawe unajua, ibilisi alienda kule, kasema, 'Nakwambia yakini naweza kumzuia asije kwenye mji huo.' Nikasema, 'Huwezi. Kama nikimwambia aende, ataenda. Nakwambia yakini angeenda. ' 'La, la, la, la, la, nitamwambia. Nitashuka niende kule na kusema, "Sasa, mawakala wangu wote, nyote kusanyikeni pamoja. Hamhitaji hata moja ya ule ushupavu wa dini wa kale hapa, uponyaji huo wote wa kale wa Kiungu na upuuzi huo wa kale wa Roho Mtakatifu. Hayo yalipita huko nyuma na mitume miaka mingi iliyopita. Mnajua hayo hayafai kitu, kule nyuma."' Akijaribu kuwapa yale magugu magumu ya kale, kila kitu namna hiyo. Wao …

97 "Lakini, unajua nini, yeye alishuka akaenda moja kwa moja kule hata hivyo. Akashuka akaenda moja kwa moja kule na kuanza kutupa nje alfalfa, kutoka … Nawe unajua nini, hao kondoo walianza kula, wananenepa wawezavyo kuwa. Naam, Bwana. Wakati wanapokuwa na uponyaji na mikutano na, Unajua, wengi wa hao jamaa wadogo wanaanza. Mbona, waliona kwamba kama wangalipata tita kubwa la nyasi kavu kama za alfalfa. Unajua walifanya nini nayo? Ilikuwa nzuri sana hata wakawakimbilia majirani, wakasema, 'Onjeni Hili! Onjeni Hili! Onjeni Hili!' Unaona, mazingira ya kule yalionekana tu kama haya papa hapa. Hili hapa papa hapa. Hili papa hapa, mnaona. 'Tubuni tu, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina Lake Yesu, mnaona, mumpokee Roho Mtakatifu. Ni kwa ajili ya ye yote atakaye, na aje, na aje hapa aone kile Biblia ilichosema. ' Unaona? Nao wana wakati mzuri sana kule chini."

"Loo, huyo ni mwanangu! Huyo ni mvulana Wangu. Vema, unafikiri amekomaa vizuri?"

98 "Ndiyo. Hakika amekomaa," kasema Roho Mtakatifu. "Nimempa majaribio. Jamani, nilimjaribu namna *hii*, nikamjaribu namna *ile*. Nimemtupa chini, mgonjwa, nimemshusha. Nilimkanyaga, nikamwacha ibilisi amfanyie kila kitu ambacho angeweza kufanya, akarudi moja kwa moja tena. Yeye alikuja hata hivyo. Unaona, akaamka tena. Nilimfanya mgonjwa. Nikafanya *hili*. Nilimtupa hospitalini. Nilimtoa hapa nje na kufanya *hivi*, nikafanya *vile*. Nilimfanya mkewe amchukie, nikawafanya majirani zake wamchukie, nikapindua kila kitu. Hilo halikuleta tofauti yoyote. Kasema, 'Ajaponiua, bado nitamtumainia.' Nikaiangamiza familia yake. Nilimchukua *huyu*, nikafanya *hivi*, nikafanya *haya* yote, nikafanya *hivi*, *vile*, *vinginevyo*. Bado alisimama imara moja kwa moja, 'Ajaponiua, bado nitamtumikia! Yeye ni wangu!'"

"Loo! Vema, ninaamini inatupasa Sisi kumwita mahali fulani maalum kidogo tupate kumfanya mwana mwenye mamlaka."

Sasa, wakati baba, katika Agano la Kale, alipofahamu kwamba mwanawe amekwisha kukomaa, na alikuwa amekwishaiva kuweza kufanywa mwana mwenye mamlaka. Kuweza! Wao huzaliwa wakiwa watoto, lakini, wakati wao ni wana papo hapo. Lakini basi hawatakuwa zaidi ya mtoto tu, mwana wa kawaida tu, mpaka watakapopevuka na kuonyesha wao ni akina nani. Ndipo, yeye anamwita nje wakati huo.

99 Sasa ni hivi, kanisa. Mko tayari? Sasa muda umeenda kidogo, kila mtu na aume kidole chake, finya nafsi yako, na ufanye moyo wako thabiti, kwa muda kidogo tu. Unaona? Sasa tutaliweka kanisa mahali pake. Sasa wakati kanisa linapofika mahali hapo, Yeye anasema, "Wamanase, mahali penu ni hapa. Efraimu, ninyi upande huu."

Ndipo anamchukua na kumpeleka mahali fulani, baba hufanya hivyo, naye anamweka mahali pa juu namna hii, naye anafanya sherehe, nao wote wanaku karibu. Naye akasema, "Nataka kila mtu ajue ya kwamba huyu ni mtoto wangu, nami nimpa mwanangu mamlaka. Nami namtaka mtu yeyote ajue, tangu sasa, kwamba jina lake … Ninamvalisha, namvisha vazi maalum. Nami nawatakeni mjue ya kwamba jina

lake ni kamili tu kwenye hundi yoyote kama jina langu lilivyo. Yeye ni mtoto wangu, mimi namfanya mwana mwenye mamlaka katika familia yangu, ingawa amekuwa mwanangu tangu alipozaliwa. Tangu alipompokea Roho Mtakatifu, amekuwa mwanangu. Lakini sasa nitamweka mahali pake katika mamlaka. Anayemfukuza kazi amefukuzwa, anayemwajiri kazi ameajiriwa:

"Na, amini, amin, nawaambieni, ukiuambia mti huu, ukiuambia mlima huu, 'ng' oka,' na usitie shaka moyoni mwako, bali uamini kwamba yale uliyosema yatatimia, unaweza kupata yale uliyosema." Unaona? Haya basi; Haya basi. Unaona? "Yeye ni mwanangu." Ni wangapi wanaojua ya kwamba kufanywa mwana mwenye mamlaka, ya kwamba ninii… walimfanya mwana mwenye mamlaka baada ya yeye kuthibitishwa kuwa ni… Kila mtu aliyewahi kuisoma Biblia, kuwekwa kwa mwana mahali pake.

100 Sasa, Mungu alimfanyia Mwanawe jambo lile lile alipompeleka Yesu juu ya Mlima wa Kugeuzwa. Aliwachukua Petro, Yakobo na Yohana kule juu, hao ni mashahidi watatu wa duniani. Kulikuwako na Yesu, Musa na Eliya, na Mungu, huko juu mlimani. Hao hapo wamesimama huko mlimani. Na, muda si muda, wao wakatazama, na Yesu akatukuzwa mbele yao. Je, hilo ni kweli? Ni wangapi wanaojua kwamba hayo ni Maandiko? Yeye alifanya nini? Yeye—Yeye alimvalisha vazi la kutokupatikana na mauti. Naye akasema, "Mavazi Yake yaling'aa kama jua." Je, hilo ni kweli? Na wingu likawafunika. Na Petro na Yohana na hao wengine, wakaanguka kifudifudi. Nao wakaangalia, na hapo wakawa wamesimama Musa na Eliya, wakizungumza Naye. Naye Musa alikuwa amekufa, na kuzikwa katika kaburi lisilo na alama kwa miaka mia nane. Na Eliya alibebwa na gari kwenda Mbinguni, miaka mia tano kabla ya wakati huo. Whiu! Lakini walikuwa wangali pale! Hao kule wakiwa wanazungumza Naye. Unaona, Yeye alikuwa amempeleka Yesu kule kuwaona, kuona mambo hayo yote yalikuwa ni nini, kuona kule, kumwonyesha Yeye mambo haya. Nao wakazungumza Naye, walifanya mazungumzo Naye.

101 Kisha mara Petro alipoangalia nyuma tena na ule utukufu ulikuwa umemwacha Yesu, walimwona Yesu pekee Yake, na Sauti ikatoka kwenye hilo wingu, na kusema, "Huyu ni Mwanangu mpendwa Wangu, msikieni Yeye! Jina Lake ni sawa tu na Langu sasa. Msikieni Yeye!" Ndiyo hiyo, kufanywa mwana mwenye mamlaka, au wana waliowekwa mahali pao.

Sasa, hapo ndipo Mungu anajaribu kulifikisha kanisa la Kipentekoste katika Kitabu cha Waefeso. Unaona? Je! Mna-mnaelewa? Hatuna budi kufunga kwa sababu tumechelewa sana, unaona, watoto wanashikwa na usingizi. Nami nilitaka kufikia hapa kwenye aya hii papa hapa, lakini siwezi kufanya hivyo, mpaka aya ya—ya 13, mnaona, sehemu ya mwisho, "kutiwa muhuri na Roho Mtakatifu wa ahadi." Tutalifikia hilo Jumapili, unaona. Angalia. Sasa, vipi, kile kinachotuingiza ni nini, na tunahifadhiwa jinsi gani na Hili.

102 Lakini sasa "kuwekwa," unawekwaje? Kwanza unazaliwa katika Ufalme na Roho Mtakatifu. Ni wangapi wanaojua jambo hilo? Vema. Halafu, umechaguliwa tangu zamani ili nini? Kufanywa mwana mwenye mamlaka. Ni kitu gani hicho? Umechaguliwa tangu zamani ili uwekwe mahali pako.

103 Loo, Dada Scott, naamini ndiye, anayeketi hapa. Si wewe ndiwe uliyekuja nyumbani leo? Fundisho fulani linaloenea mahali fulani ulimwenguni, sehemu mbalimbali nchini, nimelisikia, sana, kwamba Yesu yuko hapa duniani, akizunguka kila mahali katika mwili, Yeye anaingia na kufanya *hivi*. Huo ni uongo! Roho Wake Mtakatifu yupo hapa, Naye anajaribu kuliweka Kanisa Lake mahali pake, kuliweka Kanisa Lake katika utaratibu, kuliweka katika Nchi ya ahadi, kusudi waweze kuingia … kusudi maadui wote waweze kutupwa nje.

104 Wamanase hawawezi kuitwaa nchi yake. Siwezi kuwa na ibada ya uponyaji wakati nusu ya … wakati ninii … Ninaenda huko nje na kuhubiri ubatizo katika Jina la Yesu Kristo, na wale—na hao ndugu wa utatu wakisema, "Loo, yeye ni wa Yesu Pekee wa kale." Nami siwezi kwenda hapa na kuwa na uponyaji wa Kiungu wakati nusu yao wanasema, "Uponyaji wa Kiungu ni sawa," na wengi wao wanafurahia miujiza ya Bwana na kusema, "Vema, naamini Ndugu Branham ni nabii, lakini hebu niwaambie jambo fulani. Maadam tu Roho yuko juu yake, naye anapambanua, yeye ni mtumishi wa Bwana. Lakini Mafundisho yake yamevunda, hayafai kitu." Nani amesikia upuzi kama huo? Ama ni ya Mungu ama si ya Mungu. Hiyo ni kweli. Ama yote ni Mungu ama si Mungu. Hivyo ndivyo ilivyo. Lakini utapataje? Wamanase hatakaa kwenye ardhi yake, Efraimu hatakaa kwenye ardhi yake, Gadi hatakaa kwenye ardhi yake, Benyamini hatakaa kwenye ardhi yake, wote wanakimbizana hapa na Wafilisti, na wote wamechanganyikiwa. Sisi tutawekwaje mahali petu? Bali tumezaliwa na Roho Mtakatifu, sisi sote. Je, hilo ni kweli? Tunazaliwa kwa ajili gani? Kuchaguliwa tangu zamani … Ndipo baada ya kuzaliwa, tunachaguliwa tangu zamani kwa kufanywa wana wenye mamlaka, tupate kuwekwa mahali petu katika Mwili wa Kristo. Mnaona ninalomaanisha?

105 Mwili wa Kristo ni nini? Wengine ni mitume, wengine ni manabii, wengine ni waalimu, wengine ni wainjilisti, na wengine ni wachungaji. Sivyo? Tumeitwa hayo. Wengine wana karama za lugha, tafsiri ya lugha, hekima, maarifa, miujiza, kutenda miujiza, karama hizi zote mbalimbali. Na sasa wangefanya nini? Walifanyia mazoezi hayo kidogo. Nini? Wanaliachilia liende ovyo ovyo sijui kama nini. Mmoja anainuka, ananena kwa lugha, na huyo mwingine anaendelea, akiongea, [Ndugu Branham anaigiza sauti ya

machafuko na ghasia-Mh] A-ha. Mhubiri atakuwa akihubiri, afanye wito wa madhabahuni, na mtu fulani ainuke, anene kwa lugha na "Haleluya, Mungu atukuzwe." Kama-kama ikitokea kwamba huyo mhubiri ataendelea na ujumbe wake, kwa kuwa anao upako, basi watu watasema, "maskini mtu aliyeanguka." Unaona, ni kwa sababu hawajafundishwa.

106 Biblia ilisema roho wa manabii humtii nabii. Mungu si mwanzilishi wa machafuko. Ninaposimama hapa, ama mhudumu hapa chini ya upako wa Mungu. Haidhuru unataka kiasi gani kunena kwa lugha, tulia mpaka Mungu atakapomaliza hapa. Ndipo kama ukinena kwa lugha, haiwezi kuwa ni kurudiarudia tu kwa Maandiko, kwa kuwa Mungu alisema usipayukepayuke. Lakini ni ujumbe moja kwa moja kwa mtu fulani. Niulizeni wakati mmoja, elekeza kidole chako kwenye wakati mmoja ambapo Roho Mtakatifu aliwahi, chini ya utambuzi, kumwambia mtu fulani, alirudiarudia Andiko. Aliwaambia shida yao na yale waliyokuwa wamefanya, na jambo fulani walilopaswa kufanya au jambo fulani lililopaswa litukie, ama kitu kama hicho. Je, hiyo ni kweli?

Vivyo hivyo kunena kwa lugha na kufasiri! Kama kuna mmoja kanisani anayenena kwa lugha, na mwingine anafasiri, hebu iseme hivi. Hebu Ndugu Neville ainuke na kunena kwa lugha, na huyu ndugu hapa afasiri, aseme, "Mwambie mtu huyu hapa kwamba jana aliondoka akaenda huku nje na kufanya jambo ambalo hakupaswa kufanya. Sasa daktari alimwambia leo alikuwa na kansa. Nenda ukasahihishe jambo hilo, urudi hapa na utubu kwa Mungu."

Mtu huyo aseme, "Hakika, hiyo ni kweli." Basi Mungu yu pamoja nanyi.

107 Lakini tutalifanyaje namna hii? Unaona? Ni ninii tu, [Ndugu Branham anaigiza sauti ya machafuko na ghasia-Mh] Ni ovyoovyo tu, ni kwa namna yo yote, hakuna kuwekwa mahali petu kabisa. Sasa hiyo ni … Mnaona, Waefeso, tunajaribu … Unaona, wanakosa hilo. Mnaona jinsi wanavyolikosa? Tumechaguliwa tangu zamani ili tupate kufanywa wana na wana wenye mamlaka! Sasa ni wangapi wanaelewa ninalomaanisha, inua mkono wako juu. Kufanywa wana wenye mamlaka! Sisi tumezaliwa katika Roho wa Mungu, hakika, tunampokea Roho Mtakatifu, na kulia, "Abba, Baba! Haleluya! Utukufu kwa Mungu!" Sisi ni, hiyo ni kweli, sisi ni watoto, bali hatuwezi kufika po pote. Hatuwezi kumcharaza Mfilisti.

108 Mwangalie Billy Graham amesimama pale. Na yule Mwislamu akisema, "Thibitisha Hilo."

Mwangalie Jack Coe akiwa amesimama kule chini. Na huyo kafiri, hilo kanisa la Kristo likipeana mikono na huyo kafiri huko nje, na kumshika mkono. Anadhaniwa kuwa Mkristo, na huku anapeana mikono na ibilisi kama Joe Lewis, na mtu mwenye uhuru wa mawazo, na hata alimlaani Mungu na kusema "hakukuwako na kitu kama Mungu, kwa vyovyote, kwanza," na mambo kama hayo. Na kanisa linalojiita kanisa la Kristo, wakipeana mikono naye, nao wakiungana kumpinga Ndugu Jack Coe. Tutafanyaje chochote? Na Wapentekoste, wengi wao, wakimpinga; ambapo, kila mhubiri katika nchi yetu anapaswa kusimama naye bega kwa bega, na kusema, "Mungu, shusha Nguvu Zako." Mnaona, tuko hapo, ambapo haliwezi kuwekwa mahali pake.

109 Efraimu hataki kukaa. Mmoja wao anaenda hapa huu hapa, tunaona Wamanase wakienda kwenye sehemu hii hapa, kasema, "Loo, jamani, Bwana amenipa shamba zuri la mahindi!" Kisha huyu hapa anakuja hapa, Gadi, kasema, "Vema, sasa, ngoja kidogo. Ninapaswa kulima shayiri, bali nitapanda mahindi pia. Haleluya!" Mnaona? Huna shughuli yoyote na mahindi; lima shayiri, kazi yako ni kulima shayiri. Hupaswi kuchunga kondoo wakati unapopaswa kuchunga ng'ombe. Mungu anataka kuliweka kanisa mahali pake. Lakini kila mmoja wao anataka kufanya jambo lile lile. "Haleluya!" Wala huwezi kuwaambia kitu juu ya jambo hilo. La, la. Bado wana ile asili ya mbuzi, "Piga pembe, piga pembe, piga pembe, piga pembe, piga pembe, piga pembe, piga pembe." Unaona, huwezi kuwaambia kitu. Hiyo ni kweli. Sasa, hiyo si ni kweli? Wala huwezi kuliweka kanisa mahali pake. Unaona?

110 Kanisa linapaswa kuchaguliwa tangu zamani ili lipate kufanywa wana wenye mamlaka, ambapo mtu … Mungu anaweza kumchukua mtu na kumfanya mwana mwenye mamlaka katika familia, na kumpa kitu fulani. Hilo, kwanza, jaribu hilo uone kama ni sawa. Biblia ilisema ijaribu hiyo roho. Mtu huyu anadai jambo fulani, lijaribu uone kama ni kweli. Kama ni sawa, ambatana nalo moja kwa moja. Kisha useme, "Bwana, tutumie jambo lingine." Endeleeni kusonga mbele, mnaona, endeleeni tu kusonga mbele mpaka kila jamaa atakapochukua mahali pake. Ndipo utaona kanisa la Mungu likianza kuchukua mahali pake. Hapo ndipo Wafilisti watakapoanza kurudi nyuma. Kaptula zitaondoka, nywele zitakuwa ndefu, nyuso zitaoshwa; sigara hazitaonekana. Hiyo ni kweli. Wakati Kanisa linapoanza kuingia katika Nguvu zake kuu, wakati tuna Anania na Safira, na wachache wao. Naam, bwana. Utaona hapo hilo Kanisa takatifu limeshikamana pamoja katika Nguvu Zake, limewekwa mahali pake kama wana wa Mungu, limefanywa wana wenye mamlaka katika familia ya Mungu, Kanisa lenye nguvu likiwa limesimama pale katika utukufu wake. Loo, hilo ndilo Yeye analolijia.

111 Mnaona jinsi tulivyo mbali, ndugu? Hamwezi hata kukubaliana kwenye Maandiko. Na mtu ye yote, mtu ye yote asiyeweza kuona ubatizo wa maji katika Biblia, katika Jina la Yesu Kristo, yeye ama ni kipofu ama hana akili timamu. Hiyo ni kweli. Na hapo ndipo palipo na vita vikali.

Nita—nitamwambia mtu yeyote ambaye ataniletea Andiko lo lote ambapo mtu ye yote alipata kubatizwa katika jina lingine lo lote isipokuwa Jina la Yesu Kristo, katika kanisa jipya. Ama, kama alibatizwa kwa njia nyingine yo yote, ilimbidi kubatizwa tena katika Jina la Yesu Kristo, apate kumpokea Roho Mtakatifu. Njoo unionyeshe. Hakuna kitu kama hicho. Hakuna agizo kama hilo. Wakati Yesu aliposema kule, "Basi enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza katika Jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Baba, Mwana, wala Roho Mtakatifu, hakuna jina kati ya hayo yote, hakuna hata moja. Petro aligeuka, siku kumi baadaye, akasema, "Tubuni, mkabatizwe, kila mmoja wenu, katika Jina la Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi." Na kila mahali katika Biblia.

112 Na halafu hapa wengine walibatizwa kule chini, kwa njia nyingine, na Yohana, kwa toba tu. Paulo alisema, "Inawapasa kubatizwa tena. Inawapasa mje tena."

"Loo, lakini tumebatizwa na mtu mkuu mtakatifu, Yohana. Yeye alimbatiza Yesu."

"Vema, hii ndiyo Injili. Huyu ndiye Roho wa Mungu ambaye nimekwishafunuliwa. Mimi ni mtume wa Bwana, na kama malaika kutoka Mbinguni akija na kuhubiri kitu kingine …"

Hebu nisome hilo. Biblia ilisema, "Kama mala- …" Paulo alisema, "Kama malaika kutoka Mbinguni alisema jambo lingine lolote," askofu, askofu mkuu, papa, mwangalizi, yeyote yule, "kama akihubiri kitu kingine mbali na Hili nililowahubiria, na alaaniwe." Hakuna … Hatuna desturi kama hizo. La, bwana. Unaninii tu … Hakuna kitu kama hicho. Wewe, sisi … Na halafu—halafu, unaona, kwa nini watu hawawezi kuona jambo hilo? Kwa nini watu hawata—hawata, hawataamini jambo hilo? [Mtu fulani katika kusanyiko anasema, "Kuchaguliwa tangu zamani" — Mh.] Unaona? Mtu fulani alilipata papo hapo, Gene. "Kuchaguliwa tangu zamani," kabisa. Kwa nini? "Wote alionipa Baba wata-" (nini?) "nijia Mimi." Ni kweli jinsi gani! "Wote alionipa Baba watakuja, watakuja Kwangu." Hivi mimi nina nini, ninachojaribu kupata hapa? Tumewasili. Vema.

113 Hebu nisome tu aya hii kisha nitawaambia yale Paulo, mambo ambayo … Ujumbe ule ule niliouhubiri usiku wa leo, hivi ndivyo Paulo alivyosema juu ya kuchaguliwa tangu zamani, juu ya ubatizo wa maji katika Jina la Yesu, ubatizo wa Roho Mtakatifu, kuwekwa katika kanisa, na kadhalika. Haya ndiyo yeye aliyosema.

> *Nastaajabu* (akiwaambia hawa Wagalatia) *kwa kuwa* mmeacha *upesi hivi yeye aliyewaita … neema ya Kristo …*
>
> Nawaonea aibu sana, kwa maneno mengine, kwamba mlimruhusu mtu fulani aje na kuwavuruga akawaondoa kwenye Hilo, kugeukia injili nyingine:
>
> *Wala si nyingine; lakini wapo watu wawataabishao na kutaka* kuizuia *injili ya Kristo*, kuzuia *Injili halisi ya Kristo.*

114 Lakini angalia. Sasa, kumbukeni, Paulo ndiye aliyemsihi kila aliyekuwa hajabatizwa katika Jina la Yesu Kristo, aje na kubatizwa tena katika Jina la Yesu Kristo. Ni wangapi wanaojua hilo ni kweli? Ni wangapi wanaojua kwamba Paulo ndiye aliyesema siri hizi zilikuwa zimefichwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, na zilifunuliwa kwake, kwamba tulichaguliwa tangu zamani kuwa wana, na, kufanywa wana wenye mamlaka. Ilikuwa ni Paulo. Angalia hapa yale aliyosema.

> *Lakini ijapokuwa sisi, au malaika kutoka mbinguni, atawahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaaniwe.*

Usiseme tu, "Sikubaliani na wewe, bwana." Hebu na alaaniwe tu. Hebu nisome aya inayofuata.

> *Kama tulivyotangulia kusema, na sasa nasema tena, mtu awaye yote akiwahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo mliyoipokea* tayari, *na alaaniwe.*

115 Hiyo ni kweli. Sasa, ndugu, dada, kama ilikuwa ni Mungu hivi majuzi, na mimi—mimi nasema hilo nikitumaini kuwa si kutokuwa na kicho, ambaye alinichukua nikaone ninii ndogo … Sasa, ninasisimka; sidhani mimi husisimka, mimi hubarikiwa tu katika kuhubiri. Nashindwa kujizuia na kuwawekeni hapa mpaka ninajua mmeshikwa na usingizi na mmechoka. Lakini, loo, mimi … Kama mgali—kama mngalijua tu jinsi ninavyowatakeni muweko kule ng'ambo! Unaona? Na wakati mimi, mara ninaposema jambo hili tena, wakati mimi … wakati Yeye aliposema … Nikasema, "Ingefaa …"

Yeye akasema, "Ungetaka kuona mwisho utakavyokuwa?"

116 Nami nikaangalia nyuma nikajiona nimelala pale kitandani. Bila shaka mmenijua kwa muda mrefu vya kutosha kujua kwamba—kwamba—kwamba nawaambia Kweli. Nataka kuwaulizeni jambo fulani, kama vile Samweli alivyosema kabla hawajamtia Sauli mafuta, je! nimewahi kuwaambia lo lote katika Jina la Bwana ila lile lililokuwa kweli? Hiyo ni kweli? Daima imekuwa kweli. Je, nimewahi kuja kuwaomba fedha au kitu kama hicho? La, mnaona, sijawaomba kamwe. Je, nimewahi kufanya lo lote ila kujaribu niwezavyo kuwaongoza kwa Kristo? Kweli kabisa.

Sasa wanataka kusema mimi huwasiliana kwa mawazo, mnajua, mwonaji kiakili mwenye hisia. Bila shaka, mambo hayo hayana budi kuzuka, Biblia ilisema yangezuka. Kama vile Yambre na Yane walivyoshindana na Musa, walifanya karibu mambo yaliyofanana sana na yale Musa alilofanya, hata ilipofikia lile shindano la mwisho. Hiyo ni kweli. Lakini kumbukeni, Yambre na Yane hawakuweza kuponya. Wasingeweza kuponya. Wangeweza kuleta mapigo, bali si kuyaondoa. Unaona? Vema. Sasa, Mungu ndiye Mponyaji. Neno la Mungu linadumu kuwa Kweli.

117 Nimejaribu kuwa mwaminifu kwenu. Nimejaribu kuwaambia Kweli. Nime—nime … kwa yapata miaka thelathini na mmoja, nimesimama kwenye mimbara hii, mara huku mara kule, kwa miaka thelathini na mmoja, na siku moja huenda nikaondoka kwenda Utukufuni niiache hii mimbara. Kumekuwa na mke, binti, baba, ndugu, wote wamezikwa upande ule, marafiki wa thamani. Nimeangalia majeneza yao na maua yamewekwa hapa. Nanaujua siku moja kwamba langu litakuwa pale, pia. Sasa, hilo ni kweli. Lakini kwa uaminifu, kwa moyo wangu wote, nawaambia kwa moyo wangu wote, naamini nimewahubiria Injili ya kweli ya Bwana Yesu Kristo. Ninaamini ya kwamba mnapaswa kubatizwa, kila mmoja wenu, katika Jina la Yesu Kristo, na mpokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Na wakati wo wote mtakapofanya hivyo, utawaletea furaha, amani, uvumilivu, wema, upole, utu wema, saburi, imani.

118 Na hivi majuzi, kile kilichonipata asubuhi hiyo, sijui. Siwezi kusema kama nilikuwa hapa katika mwili mwangu na nikaona tu ono, ama kama niliondolewa hapa, hadi kule. Sijui, siwezi kusema. Jambo pekee nijualo, kwamba mimi—mimi daima niliogopa kufa, mahali hapo padogo pa mwiba. Lakini si kuogopa kwamba Yesu hangekuja kunichukua, sasa, sikuogopa jambo hilo, maana si—sikuogopa jambo hilo; bali kama ningekutana nanyi nikiwa tu ukungu mdogo wa kale unaoruka hewani. Lakini sasa naona. Nilipowaona hao watu, walikuwa halisi. Nao walikuwa watu ambao wakati mmoja walishirikiana nami hapa duniani, hata kwa mke wangu wa kwanza. Yeye hakuwa mke wangu, alikuwa dada yangu. Kamwe hakuniita mumewe, aliniita ndugu yake mpendwa. Hakukuwako na kujuana kimwili, hakuna hisia za aina hiyo, isingewezekana; ilikuwa ni kamilifu, ilikuwa ni utamu, ilikuwa ni ukamilifu.

Ninajiuliza, sijui, ninajiuliza: je, hayo ndiyo aliyoyaona, kabla hajaondoka duniani, wakati alipokuwa huko hospitalini, nilipomwita? Naye akasema, "Billy, umelihubiri hilo, umezungumza habari zake, lakini," akasema, "hujui ni kitu gani." Akasema, "Sina shauku tena ya kukaa."

119 Sijui kama hivyo ndivyo ilivyo, pamoja na yule mzee mcha Mungu, mtakatifu F. F. Bosworth, aliyesimama katika mimbara hii, ambaye amehubiri pamoja nami sehemu mbalimbali za ulimwengu. Mzee F. F. Bosworth, ninyi nyote, karibia, mlimjua; mzee mcha Mungu, mtakatifu. Masaa mawili kabla, vema, yapata wiki moja ama mawili kabla hajaondoka, nilimwendea naye akawa amelala kule nyuma, huko nyuma, karibia umri wa miaka tisini. Mikono yake midogo mizee ikiwa imenyooshwa, maskini kichwa chake chenye upara na hayo masharubu meupe usoni mwake. Nilimshika yule mzee mikononi mwangu nami nikapaza sauti, "Baba yangu, baba yangu, magari ya Israeli na wapanda farasi wake."

Kwa kuwa kama paliwahi kutokea mtu aliyewahi kuwakilisha Pentekoste na alikuwa mtume wa kweli, ilikuwa ni F. F. Bosworth, msafi, aliyenyooka, Injili halisi, unaona, ilikuwa Bosworth. Na wakati nilipomshika mikononi mwangu, nami nikapaza sauti, "Baba yangu, baba yangu, magari ya Israeli na wapanda farasi wake."

Akasema, "Mwanangu, dumu kazini." Kasema, "Wawahi vijana hawa huko nchi za ng'ambo, ukiweza, kabla hawajaingiza ushupavu mwingi wa kidini huko. Wapelekee hiyo Injili halisi uliyo nayo, mwanangu." Akasema, "Huduma yako bado haijaanza ukilinganisha na itakavyokuwa." Kasema, "Wewe ni Branham mpya kabisa." Kasema, "Wewe ni mchanga, mwanangu."

Nikasema, "Ndugu Bosworth, nina umri wa miaka arobaini na minane."

Akasema, "Hujaanza bado." Akasema, "Usiwaachie vijana hawa wahubiri wachanga wa Kipentekoste waingie kule na upuuzi chungu nzima, na kutia sumu kitu hicho, na kuwafanya wa—wajumbe wa serikali nchi nzima kulipinga Hilo kabla hujafika huko." Kasema, "Songa mbele, Ndugu Branham, endelea na Injili uliyo nayo." Akasema, "ai—naamini ya kwamba wewe ni mtume, ama nabii wa Bwana Mungu wetu."

120 Nikamwangalia, nikamkumbatia mikononi mwangu. Nikasema, "Ndugu Bosworth, nataka kukuuliza swali. Ni wakati gani uliokuwa wa furaha sana wa … wakati wako … miaka yako yote uliyohubiri?"

Akasema, "Sasa hivi, Ndugu Branham."

Nikasema, "Je! Unajua unakufa?"

Akasema, "Mimi siwezi kufa."

Nikasema, "Nini … Kwa nini ungesema huu ndio wakati wako wa furaha zaidi?"

Kulikuweko na mlango mdogo. Akasema, "Nimelala hapa huku uso wangu umegeuzwa kuelekea kwenye mlango ule. Dakika yo yote, Yeye Yule ambaye nimempenda, na Yule ambaye nimemhubiri na

kumtetea kwa, haya yote … maisha yangu, atakuja kwenye ule mlango kwa ajili yangu, nami nitaenda pamoja Naye." Nilimtazama, nikawaza, ni—nilikuwa nikimwangalia kama vile ninagalimwangalia Ibrahimu, Isaka, ama Yakobo.

Nikamshika mkono, nikasema, "Ndugu Bosworth, sisi sote tunamwamini Mungu yule yule, tunaamini jambo lile lile. Kwa neema ya Mungu nitahubiri mpaka pumzi ya mwisho itakapotoka mwilini mwangu. Nitadumu mwaminifu kwa Mungu nijuavyo kuwa. Sitapatana katika Injili kwa upande wowote au mahali po pote. Nitadumu mwaminifu nijuavyo kuwa. Ndugu Bosworth, nitakutana na wewe katika Nchi iliyo bora zaidi ambako hutakuwa kijana … ama hutakuwa mzee tena, bali kijana."

Akasema, "Utakuwakuale, Ndugu Branham, usijali."

121 Na saa moja hapo kabla, masaa wawili kabla hajafa … yapata miezi miwili baadaye, nilifikiri alikuwa anakufa wakati huo, mke wangu alikuja akamwona (daima alimpenda sana mke wangu), na halafu Bibi Bosworth. Na yapata masaa mawili alikuwa amelala, amelala usingizi. Aliamka, akaangalia, naye akaruka kutoka kitandani mwake. Akasema, "Mama, vema, sijakuona kwa miaka mingi! Baba! Ndugu Jim, mbona," kasema,"hebu tuone, ulikuwa mmoja wa waongofu wangu kwa Bwana, kule Joliet, Illinois." Alikuwa amekufa kwa miaka hamsini. Unaona? Ndio! Akasema, "Wewe ni Dada *fulani*. Naam, nilikuongoza kwa Bwana kwenye—kwenye mkutano wa Winnipeg. Naam. Mbona, huyu hapa Dada *Fulani*. Sijakuona … Naam, unaona, ulimjia Bwana mahali *fulani*." Na kwa masaa mawili mfululizo akapeana mikono na wale aliowaongoza kwa Bwana. Akarudi moja kwa moja mahali pake, akalala, akaikunja mikono yake, na mambo yakaisha. Je! Ndugu F. F. Bosworth aliingia katika ile Nchi ambayo Yesu aliniruhusu niiangalia hivi majuzi? Kama ndivyo ilivyo, yuko huko akiwa kijana mwanamume usiku huu. Mungu na aipe raha nafsi yake. Na hebu niishi mwaminifu sana daima hata nitaingia kwenye Nchi hiyo. Hebu niwe m—mtumishi wa kweli sana wa Kristo!

122 Ninayaonea maisha yangu aibu. Naona aibu. Ni—ni—ni … Kama nimefanya dhambi mbele zenu enyi watu, mna—mnaniwia mimi kuja kuniambia. Unaona? Najaribu kuishi mwadilifu katika kila kitu ambacho Mungu huniruhusu nifanye kwa neema Yake. Unaona? Unaona? Lakini, angalieni, enyi marafiki, mnaniwia mimi kama mnajua jambo lo lote ambalo ni baya maishani mwangu, njoni mniambie hivyo. Na, angalieni, ninawawia ninyi kusimama hapa na kuwahubiria Injili ya kweli. Ninawawia ninyi, kwa sababu ninatarajia kuuona uso wa kila mmoja wenu, vijana wa kiume na wa kike, kule ng'ambo ya kizingiti kile. Ni umbali wa kupumua kumoja tu kati ya mahali mlipo sasa na mahali pale. Sasa, hiyo ni kweli. Kupo.

123 Na Mungu wa neema zote, Mungu wa Mbinguni, si mwenye kukufuru, bali katika kicho, "Baba," kwenye siku ile iliyo kuu tutakaporudishwa huku na kuichukue miili yetu ya kidunia tena, ili tuweze kunywa, na kula zabibu. na matunda ya nchi. "Watajenga nyumba na mtu mwingine hatakaa ndani yake. Watapanda mashamba ya mizabibu na mtu mwingine hatakula mazao yake." Unaona? Mtu mmoja anapanda shamba la mizabibu, mwanawe analichukua, na kisha mwanawe analichukua, na jamaa yake. Bali hapa sivyo; yeye atalipanda na adumu hapo. Mnaona, hiyo ni kweli. Tutakuwa pale milele. Na hebu, katika Nchi hiyo, naomba nimwone kila mmoja wenu.

124 Nami najua kwamba humu ndani ninazungumzia hata wahudumu wa utatu. Na, ndugu zangu, sisemi jambo hili—sisemi jambo hili kusudi niudhi. Mimi ni wa utatu, pia, ninaamini katika utatu, zile sifa tatu za Mungu (Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu), bali si Miungu watatu. Unaona? Naamini kuna sifa tatu, kabisa, ninaamini hilo kwa moyo wangu wote, "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu," bali hao si Miungu watatu. Hizo ni s-...tatu tu … ama za ofisi tatu za Mungu. Mungu aliishi wakati mmoja katika Ubaba, Uwana, na sasa Roho Mtakatifu. Ni Mungu yule yule katika ofisi tatu. Nao wana …

Na Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, si Jina la Mungu. Mungu ana Jina moja, na Jina Lake ni Yesu. Biblia ilisema, "Jamaa yote Mbinguni inaitwa Yesu, na jamaa duniani inaitwa Yesu." Hiyo ni kweli. Kwa hiyo Mungu alikuwa na Jina moja, Jina la kibinadamu. Yeye alikuwa … alikuwa na jina liitwalo Yehova-yire, Yehova-rafa, hivyo vilikuwa ni vyeo vyake vya Uungu. Lakini Yeye alikuwa na Jina moja, Yesu! Na huyo Ndiye.

Na kwa kweli, ndugu zangu, kama hamkubaliani nami, kumbukeni, ni—ni—nitakutana nanyi kule ng'ambo, hata hivyo. Unaona? Nita—nitakuwa kule pamoja nanyi. Na Mungu awabariki. Nami nawapenda.

125 Nami nataka kanisa likumbuke sasa, Jumapili asubuhi tutaanzia hapa nami nitajaribu nisiwaweke zaidi ya saa nane, ili tuweze kuwa na mkutano wa alasiri, kama tukiweza, na kama nikifanya vizuri kama nilivyofanya usiku huu, saa nne na nusu. Mmenisamehe? Enyi marafiki, hatuna wakati mwingi uliosalia, wapenzi. Na—nawaiteni "wapenzi" kwa sababu ndivyo mlivyo. Ninyi—ninyi ni wapenzi wangu. Mnajua nini? Hebu … Hili hapa Andiko limekuja. Paulo alisema, "Nawaonea ninyi (Kanisa Lake) wivu, wivu wa Kiungu, kwa kuwa nimewaposea." Haya basi, inapasa liwe hivyo. Ndilo hilo. "Kwa kuwa nimewaposea, nimewaposa kwa Kristo, kama bikira safi."

126 Sasa, kama hilo lilikuwa kweli wakati huo kwenye siku hiyo, yeye alisema … Hao, hao watu waliniambia, kasema, "Yesu atakuja kwako, nawe utatukabidhi Kwake," bikira safi. "Watahukumiwa kwa

Neno ulilowahubiria.” Na, angalieni, kama nikiwahubiria yale tu Paulo aliyohubiria kanisa lake, kama kundi lake likiingia letu litaingia pia, kwa kuwa tuna kitu kile kile. Amina. Hebu na tuinamishe vichwa vyetu sasa tunaposema, “Mungu akubariki.” Sasa …?… Mchungaji wetu mpendwa, Ndugu Neville.

MESSAGE hub online

www.messagehub.info

Mahubiri Na

William Marrion Branham

"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7